# Nipashe

Jumanne Aprili 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580211

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710



## Wauawa na wananchi tuhuma kubaka, kudhalilisha wanaume

UKURASA 2




UKURASA 11

# Corona yaingia bungeni rasmi

**MBUNGE** wa kwanza athibitishwa, Dar barakoa zavaliwa kila kona, wagonjwa wapya nchini wafikia 84...*Endelea ukurasa 2,8*



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakitafuta mahitaji katika Mtaa wa Congo, jana, huku wakionyesha kuitikia agizo la kuvaa barakoa, lililotolewa na Mkuu wa mkoa huo, Paul Makonda, kwa kujifunga vitambaa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## BAA LA CORONA



Watu wanaweza kupata ugonjwa wa Covid-19 kutoka kwa wengine wenye virusi vya corona. Ugonjwa huo unaweza kuenezwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kupitia maji maji yanayotoka kwenye pua au mdomo ambayo husambaa iwapo mtu huyo mwenye ugonjwa huo atakohoa au kutoa pumzi. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## TOLEO MAALUM

## DK. REGINALD MENGI MFANO WA KUIGWA

UKURASA 3

# JPM, Wabunge wamlilia Mch. Mama Rwakatare

UKURASA 4



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play   Download on the App Store

MICHEZO   SIMBA, YANGA ZATAMBIANA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Mbunge wa kwanza apata corona

**Na Salome Kitomari,** Dodoma

UGONJWA wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona, umepiga hodi bungeni jijini Dodoma, baada ya mbunge mmoja (jina halijatajwa), kupata maambukizi.

Naibu Spika, Dk. Tulio Ackson, alisema mbunge huyo anaendelea na matibabu na kwamba afya yake inazidi kuimarika.

"Kwa muda mrefu tumekuwa tukichukua jitihada za kujiwekea tahadhari ya Covid-19 hapa bungeni, pamoja na jitihada hizi, tumepata taarifa kuwa mmoja wetu amepata maambukizi," alisema na kuongeza:

"Mgonjwa huyo anaendelea vizuri na serikali inaendelea kumpatia matibabu stahiki. Kwa mujibu wa maelezo ya mbunge huyo, alisafiri kwenda Dar es Salaam siku za karibuni, na aliporejea kuanzia Jumatano iliyopita alianza kujisikia dalili kama zilivyotangazwa na wataalamu wetu na baadaye ikathibitishwa amepata maambukizi ya corona."

Aidha, Naibu Spika aliwasisitiza wabunge kuendelea kuchukua tahadhara na kufuata maelekezo yanayotolewa mara kwa mara.

"Humu bungeni tumekuwa tukisisitizana kila wakati kwamba mbunge anayeingia bungeni ambaye ni zamu yake akae sehemu yake, asikae sehemu ya mbunge mwingine, akikaa sehemu ya mbunge mwingine, tukianza kufuatilia nani alikaa karibu na nani huyu mbunge anayezunguka na kukaa kwenye viti vya wengine atatupa wakati mgumu," alisitiza.

Aliwataka wabunge kila mmoja kuona jambo hilo lina umuhimu kama sehemu ya jamii na kama kiongozi anayetamani kujilinda na kulinda wengine.

**BUNGE KUPULIZWA DAWA**

Kwa mujibu wa Naibu Spika, baada ya kikao kuahirishwa walitakiwa kuondoka kabisa maeneo ya Bunge ili kutoa nafasi kwa ofisi na wataalamu wa Wizara ya Afya kuendelea na kunyunyiza dawa za kutakasa eneo la Bunge.

"Baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, wabunge wote kila mtu atatakiwa kuelekea nyumbani kama mlivyoshauriwa na Spika kuwa mtoke bungeni- nyumbani na nyumbani -bungeni," alisema.

**AWAONYA WABUNGE**

Aliwaonya baadhi ya wabunge wanaopeana vishikwambi (Tablet) na wengine kuhamahama kutoka eneo wanalopaswa kukaa na kutumia vipaza sauti vya wengine.

"Mbunge anaweza kuwa hayupo, lakini kishikwambi chake amemuachia mbunge mwingine na kwa hivyo mbunge huyo anapiga kura na kuonyesha kwamba mbunge huyo mwingine yupo, inaleta changamoto hasa kiofisi kwa sababu mbunge anaweza kuwa hayupo na amepata changamoto huko aliko.



Wananchi wakiwa kwenye foleni ndefu ya kwenda kupanda mabasi ya mwendokasi katika kituo cha Kimara Mwisho jijini Dar es Salaam jana. Msongamano wa abiria kwenye vituo umetokana na agizo la serikali la kuvitaka vyombo hivyo kupakia watu wanaotosha kwenye viti. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wauawa kwa tuhuma wizi, na ubakaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU wawili wanaodhaniwa kuwa ni vibaka wameshambuliwa na kupigwa na wananchi wenye hasira wilayani hapa, baada ya kutuhumiwa kuiba televisheni na ubakaji.

Watu hao waliotajwa kwa jina moja moja ni Kelvin na Chafu ambao makazi yao hayajajulikana, walipoteza maisha wakati wakiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Halmashauri ya mji wa Kahama, jana.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Majengo wilayani hapa, Vicent Assenga, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 19, majira ya saa saba mchana mtaa wa Majengo, baada ya watu hao kukamatwa na televisheni moja na radio, mali ya Ayub Kingi.

Alisema walipowakamata waliwapeleka hadi kwenye chumba wanachohifadhi vitu vya wizi na kukuta vitu mbalimbali vikiwamo vitanda na sufuria ya pilau ambayo iliibiwa siku moja kabla ya Sikukuu ya Pasaka.

Vile vile, Evarist alisema, vibaka hao walikuwa wakiwavamia wananchi nyakati za usiku na kuwaibia vitu na wakati mwingine walikuwa wakiwabaka wake za watu huku waume zao wakiangalia.

"Walikuwa wakifika kwako nyakati za usiku kabla ya chochote walikuwa wakila chakula, kumbaka mke na kisha kumuingilia kimwili mwanaume mbele ya mkewe na watoto, na kutishiwa ukienda kushtaki watauawa," alisema.

"Simu zao tulizozikamata tulikuta ujumbe wa oda mbalimbali za watu wakitaka vitanda, redio na TV," alisema.

Everist alibainisha kuwa, kijiwe chao kipo kata ya Nyasubi Phatom ambako hukutana na kupanga mikakati ya wizi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa tukio na kwamba vifo hivyo vimetokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi baada ya kuwatuhumu watuhumiwa kuwa ni wezi.

# Barakoa zavaliwa kila kona Dar

**Na Romana Mallya**

WANANCHI maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, jana waliitikia wito wa serikali wa kuvaa barakoa (mask) ili kujikinga na virusi vya corona.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliwataka wakazi mkoani humo kuanzia Jumatatu (jana) kila anayepanda daladala au anayekwenda kwenye manunuzi yoyote atatakiwa kuvaa barakoa.

Kwenye agizo hilo, Makonda aliwataka kuhakikisha wanavaa barakoa wakati wote wakiwa katika mihangaiko yao.

Alisema endapo mtu akiamua kununua, kujifunga kitambaa, kanga ni sawa ili mradi ajizibe pua yake.

Nipashe lilizunguka katika jiji hilo katika maeneo ya Kimara, Mbezi, Tegeta, Tabata Kisukuru, Magomeni, Mwananyamala na Kunduchi na kukuta mwitikio mkubwa wa wananchi waliokuwa wamevalia barakoa tofauti na siku zote.

Katika maeneo mbalimbali ya Jiji hilo, ukuwamo kwenye daladala, wananchi waliokuwa mtaani walikuwa wamevaa barakoa zinazozalishwa viwandani na zile za vitambaa ikiwa ni katika kuitikia wito huo.

Fatma Yahaya, mkazi wa Mwenge, alisema tangu serikali itangaze virusi hivyo kuingia nchini, amekuwa akichukua tahadhari zote ikiwa ni pamoja na kunawa mikono na maji tiririka kila wakati na kuvaa barakoa.

"Lazima mtu mmoja mmoja achukue tahadhari kujilinda mwenyewe na kulinda wenzake wanaomzunguka, tunapotoka nyumbani tuvae barakoa, tunawe mikono ikiwezekana tutembee na vitakasa mikono," alisema Yahaya.

Naye, John Johnson, mkazi wa Tegeta ambaye alikutwa kituo cha daladala cha Mpakani, Mwenge, akihamasisha wananchi ambao wameshindwa kununua barakoa za dukani, wanunue za vitambaa ambazo bei yake ni nafuu zaidi.

"Tusiweke visingizio, maana serikali ilipotangaza kuhusu barakoa baadhi ya watu walisema zinauzwa bei ya juu, kuna hizi za vitambaa za kushona, nimenunua tatu kila mmoja kwa Sh.1,000 na ninatembea na kitakasa mikono, pale ninapohisi nimeshika sehemu siyo rafiki ninajipaka," alisema.

Fundi wa nguo, Jumanne Seleman, mkazi wa Tandale, alisema anashona barakoa za vitambaa na kuziuza Sh. 1,000 maeneo mbalimbali.

Vilevile, Nipashe ilishuhudia katika mataa ya Ubungo, vijana wanaouza bidhaa mbalimbali wakiwa wamevaa barakoa na wengine wakiziuza za kushona.

Mbali na mwitikio huo, baadhi ya daladala katika Jiji hilo zilikuwa zikiwanyunyuzia vitasaka mikono abiria waliokuwa wakipanda.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

INVITATION TO BID (ITB)
ESTABLISHMENT OF LOCAL FRAME AGREEMENTS FOR SUPPLY AND DELIVERY OF ASSORTED ITEMS

1. Background:

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers and manufacturers to submit firm offers for Establishment of multiple Frame Agreements for the supply and delivery of any or all the below listed Items.

2. Requirement:

| TENDER REFERENCE | TENDER ITEM DESCRIPTION | DEADLINE SUBMISSION NUMBERDATE |
|---|---|---|
| ITB/2020/SUP/015 | Supply & Delivery of Spare Parts | Wednesday 13th May 2020,16.00 hours |
| ITB/2020/SUP/016 | Supply & Delivery of Toners | Wednesday 13th May 2020,16.00 hours |
| ITB/2020/SUP/017 | Supply & Delivery of Tyres | Wednesday 13th May 2020,16.00 hours |
| ITB/2020/SUP/020 | Supply & Delivery of Sanitation Products | Wednesday 13th May 2020,16.00 hours |
| ITB/2020/SUP/024 | Supply & Delivery of Pharmaceuticals | Friday 06th May 2020, 16.00 hours |

3. Eligibility:

Manufacturers, authorized resellers, wholesalers, or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

**Kindly download the tender documents in the below link:**
**https://drive.google.com/drive/folders/1bIc8pY2VnUlk8hbLbXcR4OotKTYK3g3?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to ***ndassa@unhcr.org*** copy ***ishobeza@unhcr.org***

***UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.***

215707062

TOLEO MAALUM

## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Usilie kwa kitu ambacho huna; kitumie vizuri kile ulichonacho."



# Dk. Mengi mfano wa kuigwa

**Na Elizabeth Zaya**

MOJA ya kundi linalonufaika na msaada wa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ni Chama cha Watu Wasioona (TLB).

Katibu Mkuu wa chama hicho, Emmanuel Saimon, anasema chama hicho ni miongoni mwa makundi yaliyonufaika zaidi na Dk. Mengi kwa kiwango kikubwa.

Baadhi ya vitu ambavyo Dk. Mengi aliwasaidia ni kuwaanzishia miradi ya vikundi kwa ajili ya kukopeshana.

"Sisi ni miongoni mwa watu katika jamii ya watu waliokuwa wanatuona kama hatuwezi kufanya kazi yoyote na kutuchukulia kama mzigo tu. Dk. Mengi hakuliona hilo, aliamua kutupa mtaji kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kuzalisha pesa na kutusaidia kupata mikopo ya kuazisha miradi kwa mtu mmoja mmoja,"anasema Saimon.

"Baada ya kutupatia mtaji miongoni mwa mradi tulioamua kuanzisha ni kununua gari la biashara ambalo lilitusaidia kwa kiwango kikubwa kututoa mahali tulipokuwa na kutupandisha juu kimaisha."

Licha ya gari hilo kuharibika, Dk. Mengi hakuwachoka, aliendelea kuhakikisha anawashika mkono kwa kuwaanzishia vikundi vidogo vya shughuli mbali mbali za kiuchumi ikiwamo kuwaunganisha katika vikundi vya kujiwekea akiba (Vicoba).

"Lengo la Dk. Mengi lilikuwa ni kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu nao wanakuwa na shughuli zao za kujiingizia kipato na aliamini kwamba kwenye Vicoba tutapata mikopo bila masharti na yenye masharti nafuu kwa sababu katika taasisi za benki nyingi walikuwa wanasema hatukopesheki,"anasema Saimon.

Dk. Mengi pia aliwasaidia mtu mmoja mmoja ikiwamo baadhi ya watu wenye ulemavu kulipa ada za shule na vyuo za watoto wao.

"Dk. Mengi aliamini sana elimu, japokuwa baadhi ya wenye ulemavu walikuwa wanatengwa na kufichwa ndani wasiende shule, lakini yeye ndiye aliyekuwa mkombozi wetu, alitusihi kila wakati tupeleke watoto shuleni, alipiga vita kuwaficha ndani na alijitoa kwa kuwalipia ada, iwe ni vyuo vikuu au shule za sekondari, na mpaka sasa wapo wengi ambao wako kazini kwa sababu ya msaada wake," anasema Saimon.

Anasema amesaidia kubadilisha fikra kwenye jamii ya uwezo walionao watu wenye ulemavu ambao kwa kiwango kikubwa walikuwa wanaonekana si kitu.

"Tofauti na ilivyo kwa watu wengine mashuhuri, Dk. Mengi ni mtu wa pekee ambaye alikuwa akichangamana nao pamoja na watu wa hali ya chini."



Dk. Reginald Mengi akizungumza na mmoja wa watu wenye ulemavu. **NA MPIGAPICHA WETU**

> Tofauti na ilivyo kwa watu wengine mashuhuri, Dk. Mengi ni mtu wa pekee ambaye alikuwa akichangamana nao pamoja na watu wa hali ya chini.



Katibu Mkuu wa Chama cha Watu Wasioona, Emmanuel Saimon.

Anasema pia ni daraja kati yao na serikali na mambo mengi ya watu wenye ulemavu yalizungumzwa na changamoto zao nyingi kufanyiwa kazi na serikali kupitia yeye.

Pia, alitumia vyema vyombo vyake vya habari kuhakikisha wenye ulemavu wanavitumia kupaza sauti zao na changamoto zao kusikika.

"Dk. Mengi ameamsha moyo wa Watanzania kuhusu uwezo wetu, ametufundisha tuwe wajasiriamali. Ametuachia kila kumbukumbu, tunaomba wengine waige mfano wake,"anasema Saimon.

Anasema kitabu chake cha 'I can, I must, I will' alipokuwa anakizindua, aliagiza kiandikwe pia kwa maneno ya nukta nundu ili kuwasaidia wenye ulemavu waendelee kupata mawazo yake aliyoyaacha katika kitabu hicho.

"Kwa uhakika, serikali ndiyo huwa baba au mama wa raia wake, sisi kwetu watu wenye ulemavu tulikuwa tukimchukulia Dk. Mengi kama baba yetu, alitusaidia mambo mengi, na mengi aliyokuwa akifanya yalikuwa yanaipunguzia mzigo serikali, kwa sasa hayupo, ni wakati wa serikali kuweka mkono wake kwa yote aliyokuwa akiyafanya,"anasema Saimon.

"Benki zilikuwa hazitaki kutukopesha mikopo ili tufanye biashara ndogondogo, lakini Dk. Mengi aliweka mfumo wa kutusaidia na tukawa na vikundi vya kujipatia mikopo hiyo, kwa sasa hayupo na hatuoni mwingine ambaye anaonyesha nia kutusaidia kama alivyokuwa yeye, kwa sababu serikali ndiye baba yetu tunaomba iangalie namna ya kutusaidia katika hili, tunahitaji kujishughulisha kama ilivyo kwa watu wengine."

Alitengeneza mazingira mazuri ya kuwakutanisha pamoja wenye ulemavu, serikali inapaswa kuliangalia hilo kwa kuhakikisha wanakutanishwa na kushirikishwa si kwa ajili ya chakula cha pamoja pekee bali katika mambo mbalimbali yakiwamo ya elimu, siasa na maendeleo.

Anasema serikali na sekta binafsi zinatakiwa zijifunze kutoka kwa Dk. Mengi kutokuwabagua watu wenye ulemavu katika masuala ya ajira.

Yeye aliamini kwamba kundi hilo lina uwezo kama ilivyo kwa watu wengine na hivyo kuwapa nafasi ya kuajiriwa katika kampuni zake.

"Hata kwenye kampuni zake za IPP tunaona wenye ulemavu wenye sifa za kupata ajira wamepewa nafasi, tunaomba iwe funzo kwa serikali na hata kwenye taasisi nyingine za sekta binafsi wasitubague, kama kuna wenye ulemavu wanaomba kazi na wana sifa wasiwakatae kwa sababu uwezo wanao," anasema Saimon.

# Ujenzi waanza majengo vituo jumuishi utoaji haki

**Na Lydia Churi,**
MAHAKAMA

MAHAKAMA ya Tanzania imeanza ujenzi wa majengo sita ya vituo jumuishi vya utoaji haki katika mikoa mitano nchini, ikiwa ni hatua ya Mhimili huo ya kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

Mkuu wa Kitengo cha Kusimamia Maboresho ya Mahakama (JDU), Zahra Maruma, amesema majengo hayo yameanza kujengwa kuanzia Januari, mwaka huu na yanatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 10.

Alisema majengo hayo yatakuwa na sakafu nne yaani ghorofa 3 na yatajumuisha ngazi zote za Mahakama kuanzia Mahakama Kuu mpaka Mahakama ya Mwanzo pamoja na ofisi za baadhi ya wadau wa Mahakama wakiwamo Polisi, Ustawi wa Jamii, Mawakili na Waendesha Mashtaka.

Kwa mujibu wa Maruma, majengo hayo yameanza kujengwa katika miji ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam katika wilaya za Kinondoni pamoja na Temeke.

"Kusudi la kuweka ngazi zote za Mahakama ndani ya jengo moja pamoja na ofisi za wadau ni kurahisisha na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za utoaji haki pamoja na kumpunguzia mwananchi gharama za kufuatilia huduma hizo katika ofisi tofauti ambapo humlazimu mwananchi kutumia rasilimali fedha na rasilimali muda katika kufuatilia huduma hizo."

Alisema na kuongeza:

"Upatikanaji wa huduma shirikishi katika majengo haya utampatia mwananchi fursa ya kutumia muda mchache wa kupata huduma na kumuongezea muda wa kujishughulisha katika shughuli za uzalishaji na kijamii badala ya kutumia muda huo kuzunguka katika ofisi tofauti kupata huduma za haki."

Majengo hayo yanajengwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia mradi wa Maboresho ya Huduma za utoaji haki wa kipindi cha miaka mitano.

Lengo la Mahakama ya Tanzania ni kuhakikisha kunakuwapo na Mahakama Kuu katika kila mkoa, Mahakama za Hakimu Mkazi katika kila mkoa, Mahakama za Wilaya kwenye kila Wilaya na Mahakama za Mwanzo kwenye kila Tarafa kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.



Wafanyakazi wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), wakirekebisha nyaya zilizosababisha hitilafu ya umeme maeneo ya Mtaa wa Samora Posta, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# JPM, Wabunge wamlilia Mch. Mama Rwakatare

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, wabunge wamemlilia Mbunge wa Viti Maalumu mkoa wa Morogoro, Askofu Dk. Getrude Rwakatare (70), aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana akiwa hospitalini kwa matatizo ya presha na moyo.

Mtoto wa marehemu, Muta Rwakatare aliiambia Nipashe jana kuwa, mama yao alifariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Rabininsia iliyopo Tegeta, jijini Dar es Salaam kwa tatizo la presha na moyo.

"Ni kweli mama amefariki asubuhi ya saa 11 kasoro, alikuwa na matatizo ya presha na moyo yamechanganyika pamoja kwa bahati mbaya Mungu ameamua kumpumzisha," alisema.

Muta ambaye ni Diwani wa Kata ya Kawe, alisema mpaka anakwenda mapumziko alikuwa hana hali mbaya na baadaye aliomba chakula akala na baada ya muda hali ikabadilika.

**JPM AMLILIA**

Rais John Magufuli ametuma salamu za rambirambi kwa familia, wabunge na waumini wa kanisa hilo kutokana na kifo hicho.

Alisema amesikitishwa na kifo cha mama Rwakatare ambaye alikuwa mcha Mungu, mwenye upendo, asiye na majivuno, aliyepigania umoja na amani na aliyeipenda nchi yake kwa dhati.

Rais Magufuli alimuomba Spika wa Bunge, Job Ndugai kufikisha salamu zake za pole kwa wabunge wote na pia kuwapa pole waumini wa Kanisa la Mlima wa Moto ambalo Askofu Rwakatare alikuwa kiongozi wake.

"Katika kipindi hiki cha majonzi, tumuombee Askofu Rwakatare apumzike mahali pema peponi na nawasihi waumini wa Kanisa la Mlima wa Moto muendelee kuwa wamoja na muendeleze mazuri yote yaliyofanywa na Mchungaji Rwakatare wakati wa uhai wake," alisema.

**BUNGE LASHTUSHWA**

Spika wa Bunge, Ndugai alisema amepokea kwa mshtuko na masikitiko taarifa za kifo cha mchungaji Rwakatare.

"Natoa pole kwa wafiwa wote wakiwamo familia ya marehemu, ndugu, jamaa na waheshimiwa wagunge na waumini wa kanisa la mlima wa moto, Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu na subira katika kipindi hiki kigumu," Spika Ndugai alisema katika taarifa hiyo.

Vile vile, alisema Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na familia ya marehemu inaratibu mipango ya mazishi na taarifa zaidi zitaendelea kutolewa.

Mwaka 2007 Rais Jakaya Kikwete (mstaafu) wa awamu ya nne, alimteua kwa mara ya kwanza, mama Rwakatare kuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) na Januari 28, mwaka 2008, aliapishwa rasmi.

Nafasi hiyo aliipata baada ya kifo cha aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Salome Mbatia.

Baada ya uchaguzi wa mwaka 2015, miaka miwili baadaye Rais Magufuli alimteua kushika ubunge wa viti maalum.

**WABUNGE WAMKUMBUKA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema walikuwa wakimuita 'Kisulisuli; naye alifurahia utani huo, na kwamba kifo chake ni pigo kwa Mkoa wa Morogoro na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ujumla.

Mbunge wa Viti Maalumu, Devotha Minja, alisema amepokea kwa masikitiko makubwa kama mbunge na mzazi anayesomesha watoto wake katika shule za Dk. Rwakatare, mkoani humo.

"Tumepoteza mtu ambaye tukiachana na mambo ya siasa na upinzani, alikuwa mama, mtu wa msaada mwenye huruma pamoja na fedha na vitu vyake, lakini hakuwa mtu wa kujikweza, tulikuwa tunashirikiana pamoja na alikuwa hawezi kupita bila kukusalimia hata akukute wapi,"alisema.

Kwa mujibu wa Minja, mbunge huyo anamiliki shule mbili, Morogoro mjini ambayo imekuwa ikifanya vizuri kiwilaya na kimkoa na kazi kubwa alikuwa akiifanya ni kusimamia kwa karibu ikiwamo kufanya ziara za kushtukiza.

"Kama mzazi tunaona tumepoteza mtu ambaye alikuwa na nia njema ya kusaidia watoto wetu wapate elimu nzuri, mara kwa mara alikuwa anakwenda mwenyewe kwenye ziara ya kushtukiza shuleni jambo lililosaidia sana kuifanya shule iwe bora na wazazi tufurahie kusomesha watoto," alisema na kuongeza:

"Alikuwa mama makini na aliyemaanisha, tutamkumbuka sana, tutamkosa sana, tumepoteza mtu muungwana, muda wowote ukimpigia simu anapokea."

Naye, Mbunge wa Viti Maalumu, Ritha Kabati, alisema Mama Rwakatare alikuwa mtu wa dini na kila mara wakikutana naye aliwaombea, na walipenda kumtania kisulisuli naye alicheka.

"Mimi ninavyoona ni mama aliyekuwa anaongoza kanisa kubwa, ukikutana naye anakuombea kwa mambo mengi bila kujali. Nitamkumbuka kwa maombi yake, kila ukikutana naye atakuombea na kukupa maneno ya Mungu, tunamtania kuhusu kisulisuli na anasisitiza watu kuomba kila mara, alikuwa ni mama aliyependa kumwombea kila mtu kila wakati," alisema.

Kwa mujibu wa Mbunge Kabati, Dk. Rwakatare alitumia dakika tano za muda wake wa kuchangia bungeni kuomba kwanza na ndipo aendelee.

Naye, Mbunge wa jimbo la Ulanga, Goodluck Mlinga, alisema alikuwa mama anayejitoa kusaidia kinamama mmoja mmoja au vikundi kwa kutumia fedha zake binafsi.

"Kwa upande wa chama alijitoa sana, maana alikisaidia kwa fedha, kwa kweli ni pigo kwa chama hasa katika kuelekea Uchaguzi Mkuu, mwaka huu," alisema.

Naye, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, Aeshi Hilary, alisema kwa muda mrefu alikaa naye jirani ndani ya bunge na alikuwa kiongozi mzuri aliyejali shida za watu wa kawaida.

"Alikuwa msikivu na alipenda sana kutushauri vijana tunapotaka kwenda kasi, alitushauri sana kwenye masuala ya dini na alituongoza kuwa baada ya kifo kuna maisha yanaendelea. Kuondoka kwake ni pigo kubwa sana maana umuhimu wa mtu unaujua baada ya kifo chake," alisema.

***Imeandikwa na Salome Kitomari (Dodoma) na Romana Mallya (Dar)***

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA KUPAMBANA NA VIRUSI VYA CORONA VINAVYOSABABISHA UGONJWA WA HOMA KALI YA MAPAFU (COVID-19)

***Dar es Salaam, 19 Aprili, 2020:***

Uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") unapenda kuwajulisha walipakodi na wananchi wote kwa ujumla kwamba kufuatia maagizo na maelekezo ya Serikali kutaka kila mtu kuchukua hatua za kujikinga na kuzuia maambukizi mapya na kuenea kwa ungonjwa wa Corona (COVID-19) kwa kuwalinda watumishi pamoja na wadau, TRA inatoa maelekezo yafuatayo:-

1. Kuanzia siku ya Jumatatu tarehe 20 Aprili 2020 (na kuendelea) wageni wote watakaolazimika kufika katika Ofisi za TRA kote nchini, ili kupata huduma mbalimbali,watatakiwa kuvaa barakoa (mask) kwa lengo la kujikinga wao wenyewe na kuwakinga wenzao na kuzuia maambukizi mapya ya ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (COVID-19);

2. Ili kupunguza msongamano, TRA inawahimiza walipakodi na wadau wengine kutumia njia mbadala za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kupiga simu bure (0800-750075 au 0800-780078), kutuma ujumbe wa WhatsApp (0744-233 333), barua pepe (huduma@tra.go.tz), na kutembelea tovuti yetu (www.tra.go.tz) ili kupata baadhi ya huduma zetu kwa njia ya mtandao na taarifa mbalimbali; na

3. Walipakodi wote watatakiwa kuzingatia maelekezo ya kujikinga na kuwakinga wengine kama inavyoelekezwa na Wizara ya afya mara kwa mara ikiwemo kunawa mikono na kupaka vitakasa mikono (sanitizers) wakati wa kuingia na kutoka kwenye Ofisi zetu.

Mamlaka itaendelea kuzingatia tahadhari zote dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 pasipo kuathiri utendaji wa kazi (business continuity) zetu na kuwahudumia wateja. Kwa namna ya kipekee, TRA inawashukuru walipakodi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia kwa kulipa kodi ya Serikali kwa hiari kama ilivyo matakwa ya Sheria.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI MAKAO MAKUU**

215708202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Bravo wakazi Dar kuitikia agizo la Makonda, lakini...

**KATIKA** hali inayoonyesha kwamba elimu inayoendelea kutolewa nchini na serikali pamoja na wadau kwa umma, kuhusu hatua za kuchukua kujiepusha na maambukizi ya homa kali ya mapafu COVID-19, inayosababishwa na virusi vya corona imeeleweka , jana wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, walionyesha hilo kwa vitendo.

Wiki iliyopita, Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, aliwaagiza kila mmoja kuvaa barakoa kila mahali anapokwenda ikiwamo, kazini, katika biashara, naeneo ya huduma na msisitizo ukawekwa kwa wanaotumia usafiri wa daladala.

Jambo la kufurahisha na kutia moyo ni kuwa wakazi wengi wa maeneo mbalimbali jijini jana waliitikia wito wa serikali wa kuvaa barakoa (mask) ili kujikinga na virusi vya corona.

Kwa mujibu wa agizo la Makonda, kila mkazi alitakiwa kuanza kulitekeleza juanzia jana, na hakika makundi makubwa ya wakazi walionekana kulitekeleza.

Wakati anatoa agizo hilo, alisema endapo mtu akiamua kununua, kujifunga kitambaa, kanga ni sawa ili mradi ajizibe pua yake.

Gazeti letu katika ufuatiliaji wake katika maeneo kadhaa ya Jiji, lilishuhudia mwitikio mkubwa wa wananchi waliokuwa wamevalia barakoa tofauti na siku zote.

Katika maeneo mbalimbali ya Jiji, ikiwamo kwenye daladala, wakazi waliokuwa mtaani walikuwa wamevaa barakoa zinazozalishwa viwandani na zile za vitambaa ikiwa ni katika kuitikia wito huo.

Baadhi ya wakazi waliunga mkono agizo hilo, wakisema ni muhimu kama tahadhari kujilinda mwenyewe na kulinda wenzake wanaomzunguka.

Baadhi waliwahamasisha wakazi wengine ambao hawajaona umuhimu huo na kuanza kuchukua hatua za tahadhari, kuanza mara moja ukiwamo kuvaa barakoa, kunawa mikono na ikiwezekana tutembee na vitakasa mikono.

Kwa upande mwingine, mkazi mmoja wa Tegeta alikutwa kituo cha daladala cha Mpakani, Mwenge, akihamasisha wananchi ambao wameshindwa kununua barakoa za dukani, wanunue za vitambaa ambazo bei yake ni nafuu zaidi.

Alitoa angalizo kuwa wakazi wasiweke visingizio, maana serikali ilipotangaza kuhusu barakoa, baadhi ya watu walisema zinauzwa bei ya juu, lakini kuna za vitambaa za kushona, na kuwa amenunua tatu kila mmoja kwa Sh. 1,000, na kuahidi kuendelea na kitakasa mikono, pale anapohisi ameshika sehemu siyo rafiki anajipaka.

Tunampongeza Makonda kwa kubuni wazo hilo na kulitoa kama agizo kwa kila mkazi wa Mkoa huo.

Aidha, ni jambo la kuwapongeza wakazi wa Jiji hilo kwa mwitikio mkubwa waliouonyesha, na hii inadhihirisha kuwa kila mmoja anajali maisha yake na ya wengine.

Kimsingi, utekelezaji wa agizo la kuvaa barakoa unapaswa kuwa jambo la kudumu kwa kila mmoja kwa ajili ya usalama wake, wa wenzake na taifa kwa ujumla.

Tufike mahali sasa tubadilike kwa kutii sheria, kanuni, taratibu, miongozo na maelekezo yanayotolewa na mamkala zetu. Kwa lugha nyingine, kila mmoja anapaswa kutii sheria bila shuruti.

Tunashauri utamaduni wa kuvaa barakoa na hatua nyingine zinazoelekezwa na serikali pamoja wataalamu wa afya ukawe endelevu hadi hapo ugonjwa huo utakapodhibitiwa kabisa.

Hata hivyo, kwa kuwa bado kuna wasiwasi kuhusiana na aina gani ya barakoa zina viwango vya ubora pamoja na wananchi wa kawaida kutokuwa na uwezo wa kuzipata, tunaishauri serikali ilichukua suala hili kama changamoto, halafu ilipatie ufumbuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Corona inapogeuzwa kisingizio udhalilishaji watu mitandaoni

Na Beatrice Moses

**UGONJWA** wa corona ni tishio duniani. Nchi mbalimbali zinahaha jinsi ya kudhibiti virusi vya COVID-19, ambavyo tayari vimesababisha vifo vya watu 166,051 na wengine takribani milioni 2.4 wameugua na baadhi hawajui hatima ya maisha yao, licha ya kwamba wapo waliopona.

Jambo la kushangaza ni kwamba, baadhi ya watu wamechukulia ugonjwa huo kama jambo la mzaha wakijiburudisha kwa kufanya masihara, huku baadhi wakitumia vibaya simu zao kutoa taarifa ambazo si za kweli zikielezea vifo vya wengine.

Watu hao baadhi yao wamekuwa wakiwazushia vifo ama kutaja majina ya wagonjwa jambo linlozua hofu na usumbufu kwa jamii.

Tanzania kama nyingine inaongozwa kwa mujibu wa katiba, sheria na taratibu, ndiyo maana Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ndiye mwenye dhamana ya kutoa taarifa kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini.

Ni vyema kukumbushana kuwa sheria zipo mathalani ya Makosa ya Mtandao 2015, pamoja na mambo mengine imetajwa kuwa imetokea, baada ya ukuaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kukua kwa kasi nchini Tanzania.

Katika sheria hiyo kifungu namba 12, pamoja na mambo mengine kinazuia pia uchapishaji wa "maudhui ya uongo ambayo yanaweza kutapeli au kudanganya jamii isipokuwa ambapo maudhui hayo yameandikwa kuwa ni (i) kiburudani ( ii)kutungwa na (iii) ambapo yametanguliwa na maelezo kuwa maudhui hayo si ya kweli".

Kwa sababu za usalama wa taifa na usalama wa raia, kifungu namba 12 (1) (j) kinazuia usambazaji wa taarifa zinazohusiana na mashambulizi ya kigaidi na milipuko ya magonjwa,

Pamoja na kuwa baadhi ya taasisi zinakosoa sana uwapo wa sheria hizo zikieleza kuwa jamii inapaswa iwe na taarifa hizi ili iweze kujizatiti ipasavyo.

Kulingana na kifungu namba 16 cha sheria hiyo, kinatoa adhabu sawa kwa wahukumiwa wote, lakini pia kuna ya faini isiyopungua Sh. 5,000,000 au kifungo kisichopungua miezi 13 au vyote kwa pamoja.

Upashanaji wa habari inaweza kuwa na wigo mpana lakini haiondoi ukweli kwamba ni fani mojawapo muhimu kwa jamii, ambayo ikitumiwa vizuri inasaidia katika kuiletea nchi maendeleo, pia inapotumika vibaya inahatarisha usalama wa nchi na raia kwa ujumla.

Ni vyema watumiaji wa simu za mkononi hasa simu janja (smart phones) kutambua mipaka yao na kuheshimu sheria kwa ujumla ili kuepuka kuingia kwenye majanga ambayo wanakuwa wameyatengeneza kwa mikono yao wenyewe.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeshatoa maonyo kadhaa kwa viongozi wa makundi ya mitandao ya kijamii ikiwamo WhatsApp, huku ikiagiza wanavikundi kuwaripoti wale wanaozusha ama kurusha taarifa za uongo kwenye makundi.

Wakati huu , wanajamii wanapaswa kuwa makini na taarifa wanazozisoma ama kuzirusha kwenye mitandao ya kijamii na siyo vyema kurusha mambo ambayo hawana uhakika nayo.

Hivi karibuni kuna taarifa zilieleza kuwa mwanahabari mmoja amefariki kwa ugonjwa huo, hali hiyo ilisababisha mateso kwa baadhi ya ndugu jamaa na marafiki.

Pengine kwa kuona na kutambua jinsi ambavyo habari hiyo ya uongo ilivyosumbua wengi, hatimaye mwandishi huyo aliamua kujirekodi video akijionyesha alivyo mzima kwa neema ya Mungu, hatua ambayo ilisaidia kukomesha uzushi dhidi ya kifo chake.

Ni vyema kukumbushana kuwa sheria ya kukomesha wazushi wa mitandaoni ipo na imewekwa ili kuzuia mambo kama hayo, hivyo anayeamua kurusha habari ambazo hana uhakika nazo ni wazi kuwa ameamua kufanya makosa ili akumbane na adhabu inayomstahili.

Matumizi mazuri ya simu ni pamoja na kusambaza taarifa zilizo sahihi, katika kipindi hiki ni vyema ikitumika katika kurusha habari zinazosaidia jamii katika kupata uelewa wa namna ya kujikinga na maambukizi mapya.

HABARI

# Ufaransa yasaidia Afrika vita corona

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI maambukizi ya virusi vya Corona yakizidi kuongezeka kwenye nchi za Afrika, Ufaransa imetangaza kuongeza nguvu katika kuzisaidia nchi za bara hilo, Tanzania ikiwamo katika mapambano hayo.

Taarifa iliyotolewa jana na serikali ya Ufaransa kupitia kwa Balozi wake nchini, Frederic Clavier, ilisema kuwa kupitia Shirika lake la Maendeleo (AFD), imetenga kiasi cha Euro bilioni 1.2 kupambana na corona Afrika.

Katika taarifa hiyo, Balozi Clavier alisema jitihada hizo zinalenga kwenye utafiti na kuimarisha mifumo ya afya katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Huu ni mpango wa serikali ya Ufaransa kuhakikisha nchi za Afrika zinapambana na janga hili, lakini pia kupambana na mtikisiko wa kiuchumi unaotokana na mlipuko wa virusi vya corona," alisema Clavier.

Alisema kwa Tanzania mbali na fedha hizo kusaidia mapambano ya corona, pia Ufaransa imezitaka kampuni za Kifaransa na wafanyabiashara kuunga juhudi za Serikali ya Tanzania katika kupambana na virusi vya corona kwa kutoa vifaa kinga vya kupambana na virusi hivyo.

Kwa muda mrefu Ufaransa kupitia AFD, imekuwa ikizisaidia nchi za Afrika katika nyanja mbalimbali, ambapo kwa mwaka 2019 pekee, imetumia Euro bilioni 11 na kuwa nchi ya tano duniani miongoni mwa nchi zilizotoa msaada.




Mwakilishi wa mauzo wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) Mkoa wa Kagera, Laurent Nditi (kulia), akikabidhi sehemu ya vipeperushi vyenye ujumbe wa namna ya kujikinga na virusi hatari vya corona kwa Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Hassan Kawia. SBL imejitolea kwa kushirikiana na Wizaya ya Afya kusambaza vipeperushi hivyo nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Matatani madai kukutwa na dawa za kulevya nyumbani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHIKU Tungu (57), mkazi wa Majengo Kambarage, Manispaa ya Shinyanga na wenzake watatu, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya nyumbani kwake.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimbа, alisema watu hao wanne walikamatwa kwa pamoja wakiwa nyumbani kwa Chiku wakiwa na dawa hizo.

Aliwataja waliokamatwa na dawa hizo ni Hassani Ibrahimu (22), Juma Omary (26), Abdallah Hemed (23), na kuwa walikutwa nyumbani kwa Chiku Tungu, wakiwa ndani ya uzio wa nyumba yake wakiwa na dawa hizo.

"Majira ya saa sita mchana jana (juzi) katika Mtaa wa Majengo Kambarage, askari baada ya kupata taarifa za kiintelinjensia, walifika nyumbani kwa mtuhumiwa Chiku, na kuwakamata watuhumiwa wote wakiwa na dawa za kulevya ndani ya uzio wa nyumba yake," alisema Magiligimba.

"Dawa za kulevya tulizowakamata nazo ni pinchi nane za heroine, rizla, kigae cha kusugulia dawa, pamoja kisu kimoja, na watuhumiwa wote wapo mbaroni wanahojiwa kwa kina, na watafikishwa mahakamani," aliongeza.

Aliwaomba wananchi mkoani Shinyanga, kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi, kwa kutoa taarifa mbalimbali za kiuharifu pamoja na uuzwaji wa dawa za kwa kulevya, ili watuhumiwa wakamatwe.

# Kizimbani tuhuma wizi K-Vant katoni 1,182

**Na Hellen Mwango**

MTUNZA stoo, Rashidi Muhina (45), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na shtaka la wizi wa pombe kali aina ya K- Vant katoni 1,182 zenye thamani ya Sh. milioni 103.9, mali ya Kampuni ya Mega Bevarege LTD.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka ya mshitakiwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Wakili wa Serikali, Kija Luzungana, alidai kuwa siku tofauti kati ya Aprili Mosi, mpaka Juni 30, 2019 mtaa wa Togo Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Kampuni ya hiyo, aliiba katoni 1,182 za K-vant zenye ujazo wa gramu 750 zenye thamani ya Sh.103,928,000, mali ya mwajiri wake.

Luzungama alidai kuwa mshtakiwa aliiba mali hizo kupitia nafasi yake kama mtunza stoo. Hata hivyo, mshtakiwa alikana tuhuma hizo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika, hivyo uliomba tarehe nyingine ya kumsomea mshtakiwa amaelezo ya awali.

Hakimu alisema mshtakiwa atakuwa nje kwa kutimiza masharti ya dhamana ya kutoa fedha taslimu Sh.milion 51 au hati ya mali isiyohamishika, yenye thamani hiyo, wadhamini wawili watakaosaini hati ya dhamana ya Sh. milioni 26 kila mmoja.

Hata hivyo, mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti hayo, hivyo kupelekwa mahabusu mapaka Mei 4, mwaka huu, ambapo atasomewamaelezo ya awali.


## JOB VACANCY

Applications are invited from suitably qualified persons to fill the following post: -

**DIRECTOR OF FINANCE AND BUSINESS DEVELOPMENT**

The Director of Finance shall be the Head of Directorate of Finance and Business Development and is responsible to the Director General. He shall direct and coordinate the organization's financial resources.

**In Finance**
- Supervises the implementation of accounting functions by ensuring collection, classification, recording and reconciliation of accounting data.
- Reviews constantly the organization's financial position and ensures prompt provision of relevant financial information to Management.
- Takes appropriate action for collecting revenue due to the Organization.
- Ensures that the organization timely meets its financial obligations and all payments are made in accordance with financial regulations and under appropriate authority.
- Ensures prompt production of accurate Annual and Financial reports for auditing and publication in accordance with the statutory requirements.

**In Business Development**
- Responsible for overall management of all strategic and operational marketing activities.
- Plans and coordinates implementation of business plans and penetration to new markets.
- Coordinates customer care trainings to all staff placed at the organization.

**QUALIFICATIONS AND EXPERIENCE**
Holder of a Masters Degree in Finance/Accounts/Commerce, a CPA (T) or an equivalent full professional accountancy qualification plus at least 3 years working experience in accounting or audit practice at a senior level. Registration with NBAA as authorized accountant is essential.

**SALARY AND FRINGE BENEFIT**
An attractive salary will be given to the right candidate.

**WORK STATION**
Dar-es-Salaam, Tanzania.

**Dead line: 04.05.2020**

**MODE OF APPLICATION**
Applications accompanied with photocopies of relevant certificates and testimonial should be sent to the address below so as to reach them within fourteen days from the date of first press appearance of this advertisement.

All applications should be submitted at the physical address provided below:

**The Guardian Ltd,**
**Mikocheni Industrial Area, Dar es Salaam**
**Voucher Number: 01**

215708602




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (wa tatu kushoto), akitoa shukrani kwa kampuni ya Bima ya Sanlam, baada ya kupokea hundi ya Sh. milioni 172.5 zilizotolewa na kampuni ya Bima ya Sanlam Life Insurance na Sanlam General Insurance kusaidia juhudi za serikali katika kupambama wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya Corona (covid-19), katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kutoka kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu wa Sanlam Life, Charles Mbaga, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam Life, Khamis Suleiman, Mwenyekiti wa Bodi wa Sanlam, Balozi Dk. Matern Lumbanga, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam Kanda ya Mashariki, Julius Magabe na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sanlam Genral Tanzania, Gift Noko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Anayedaiwa kujifanya ofisa wa Nida alivyotiwa mbaroni

**Na Hadija Maloya**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), imewataka wananchi kuacha kutumia vishoka wakati wa mchakato wa kuomba Vitambulisho vya Taifa na kuwataka wafuate utaratibu rasmi uliowekwa na serikali wa kuomba vitambulisho hivyo.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Geofrey Tengeneza, alitoa tahadhari hiyo kufuatia tukio la mwananchi mmoja (jina limehifadhiwa), mkazi wa Kigogo Fresh jijini Dar es salaam, kufika ofisi ya Nida wilaya ya Ilala, iliyoko Ukonga Mombasa, kupiga picha ya kibaometriki kwa ajili ya Kitambulisho cha Taifa na kuwadokeza maofisa usajili wa Nida kuwa baada ya kukamilisha upigaji picha alielekezwa na mtu mmoja kupeleka fomu yake ya maombi kwake ili amkamilishie vipengele vilivyobaki pamoja na kumpatia cheti cha kuzaliwa.

Mwananchi huyo alisema fomu yake ya maombi ya kitambulisho hicho pia ilisainiwa na kugongwa muhuri na mtu huyo na kumpatia barua baada ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa anakoishi wa Kigogo Fresh kukataa kutoa barua na kusaini fomu zake kutokana na kutokuwapo kwa cheti cha kuzaliwa kama utaratibu unavyotaka.

Mtuhumiwa huyo alitiwa mbaroni na kisha kufanyiwa upekeuzi kwenye ofisi yake katika duka moja la steshenari lililoko Ukonga Mombasa, ambako walikuta nyaraka mbalimbali za serikali zikiwamo nakala za fomu za maombi ya vitambulisho vya taifa (FIA) ambazo tayari zimegongwa muhuri, nakala za hati za kiapo cha kuzaliwa (Affidavit form) na nakala za barua za utambulisho wa makazi zenye muhuri wa ofisi ya Serikali ya Mtaa wa Mwembe Madafu.

Mtuhumiwa huyo ambaye jina lake limehifadhiwa, tayari amefunguliwa mashtaka kwa kosa la kukutwa na nyaraka za serikali kinyume cha sheria na kosa la kujifanya ofisa wa Nida.

Akizungumzia tukio hilo, Tengeneza alisema mtu huyo atakuwa ni kishoka ambaye bila shaka hata muhuri wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa aliogonga na barua ya Serikali ya Mtaa aliyoitoa kwa mwananchi huyo ili awasilishe katika ofisi ya Nida Wilaya ya Ilala kwa ajili ya kupatiwa Kitambulisho cha Taifa, vitakuwa feki.

Alionya watu wanaojihusisha na kuwarubuni wananchi waache tabia hiyo kwa kuwa Mamlaka haitasita kuwachukulia hatua kali za sheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

# UVCCM kuongoza mapambano dhidi corona

**Na Maulid Mmbaga**

UMOJA wa Vijana (UVCCM) jijini Dar es Salaam, jana umezindua mkakati maalumu wa kuzuia maambukizi ya homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) mkoani humo.

Mkakati huo uliongozwa na Mwenyekiti, Mussa Kilakala, aliyekutana na viongozi wa Umoja huo wa wilaya tano za Mkoa wa Dar es Salaam na kuwapa dira namna ya kuendesha hamasa hiyo kwa weledi huku wakizingatia ushauri wa wataalamu wa afya kujikinga na ugonjwa huo.

Katibu wa hamasa wa Umoja huo mkoani humo, Ally Mohammed, alisema ugonjwa wa corona ni wa kisayansi na umoja huo umeonyesha njia na inapaswa kuigwa na vijana wote nchini bila kujali itikadi zao.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO), maambukizi ya corona huenda yakashika kasi katika bara la Afrika kutokana na udhaifu wa huduma za kiafya.

"Ugonjwa huu tutaukomesha kwa kuwa na umakini na nidhamu ya hali ya juu katika kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya, kunawa mikono kwa maji yanayotiririka kwa sabuni, kupaka vitakasa mikono (Sanitizer) na kuvaa barakoa kila tunapotoka majumbani mwetu," alisema.

Aliongeza kuwa, katika operesheni hiyo waligawa vifaa vya kujikinga na corona kwa viongozi wa umoja huo ngazi ya wilaya, na kutembelea maeneo ya soko la Feri na kugawa kwa vitakasa mikono kwa madereva bajaji na pikipiki, na kutoa tangi la maji kwa uongozi wa soko hilo.

Vile vile, alisema zoezi hilo ni endelevu na kutoa wito kwa wadau kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na maambukizi ya Covid-19, hasa Mkoa wa Dar es Salaam ambao unaongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa wa corona nchini.

# Wagonjwa wapya corona 84 wagundulika

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya wagonjwa wa virusi vya corona nchini imezidi kuongezeka hadi 254, baada ya jana kubainika wagonjwa wapya 84.

Taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ilieleza kuwa kati ya ongezeko hilo, wagonjwa 16 ni waliotolewa taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar jana.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa upande wa Tanzania Bara idadi ya wagonjwa hao wanatoka mikoa ya Dar es Salaam (33), Arusha (4), Mbeya (3), Kilimanjaro (3) na Pwani (3).

Wengine ni kutoka Tanga (3), Manyara (2), Tabora (1), Dodoma (3), Ruvuma (2), Morogoro (2), Lindi (1), Mara (1), Mwanza (3), Mtwara (1), Kagera (1) na Rukwa (2).

"Wagonjwa wote walioripotiwa Tanzania Bara wanaendelea vizuri, isipokuwa wagonjwa wanne wanaopatiwa huduma za wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum," ilieleza taarifa hiyo na kuongeza:

"April 18, mwaka huu, Waziri wa Afya wa Zanzibar alitoa taarifa ya uwapo wa wagonjwa 23, ongezeko la wagonjwa wapya linafanya idadi ya watu waliopata maambukizi ya ugonjwa wa corona nchini kufikia 254 kutoka wagonjwa 147, tuliowatolea taarifa April 17."

Taarifa hiyo ileleza kuwa, kumetokea vifo vitatu katika Jiji la Dar es Salam, ambao wamethibitishwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

# RC awaombea wanahabari vifaa kinga ya corona

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali Emannuel Maganga, amemuomba Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Simon Chacha, kufanya utaratibu wa kutoa vifaa kinga vya ugonjwa wa corona kwa waandishi wa habari mkoani hapa.

Maganga aliyabainisha hayo mwishoni mwa wikim wakati akitoa taarifa ya mwenendo wa kujikinga na ugonjwa wa huo mkoani Kigoma na kusema kuna haja ya kuwekwa utaratibu kwa waandishi wa habari kupata barakoa watakazozitumia wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

"Katibu wa chama cha waandishi wa habari ufuatilie suala hilo, mnapaswa kujikinga kwani mnakutana na watu wengi halafu pia wakati mwingi tuko na nyie," alisema.

Vilevile Maganga alibainisha kuwa, hali ya uelewa wa wananchi katika kujikinga mkoani humo ni nzuri kwani wananchi wanazingatia kunawa mikono na kuchukua tahadhali wanazoshauriwa na watalamu wa afya.

Hata hivyo, alieleza kwa sasa changamoto iliyopo ni wananchi kuendelea kusongamana katika maeneo ya masoko na kueleza kuwa bado wanahangaika kupata namna bora ya kutatua suala hilo ili wananchi waendelee kuwa salama

"Hawa ni wananchi wetu, hatupendi kutumia nguvu zaidi hivyo tunajikita kutoa elimu kwao, lakini kama njia hiyo haita kuwa na mafanikio tutalazimika kutumia njia nyingine ili wafuate maagizo kwa lazima," alisema.

Naye Dk. Chacha alisema amepokea ushauri wa mkuu wa mkoa naataufanyia kazi hivi karibuni baada ya taratibu muhimu za upatikanaji wa vifaa hivyo kukamilika.

Pia alieleza katika mwendelezo wa udhibiti wa ugonjwa wa corona, wameendelea kuongeza umakini katika maeneo ya mipakani, kutokana na kuwa na muingiliano na raia wa nchi jirani unaosababishwa na shughuli za kibiashara.

Utoaji taarifa ya mwenendo wa udhibiti ugonjwa wa Corona uliambatana na upokeaji vifaa vya Tehama na samani vitakavyotumika katika ukusanyaji wa taarifa za ugonjwa huo vyenye thamani ya Sh.105,0000,000 kutoka shirika lisilo la kiserikali la Management and Development health Tanzania ( MDH) kupitia ufadhili wa Taasisi ya Udhibiti wa Magonjwa ya Marekani.

# Tuhuma uuzaji pembejeo zaizindua Bodi ya Pamba

**Na Shaban Njia, KISHAPU**

KUTOKANA na malalamiko ya wakulima wa pamba wilayani Kishapu mkoani Shinyanga ya kuwatuhumu viongozi wa Vyama vya Msingi (AMCOS) kuuza pembejeo zilizolewa na serikali kwa mkopo kwa wakulima, Bodi ya Pamba Tanzania imezinduka na kuanzisha msako mkali katika maduka ya pembejeo.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuanza msako huo juzi, Mkaguzi wa Bodi ya Pamba, Thomas Daudi, alisema watafanya ukaguzi kwenye maduka ya pembejeo ya watu binafsi, minada na magulio yote wilayani humo ambayo pembejeo hizo huuzwa kwa wakulima.

**Niwatake viongozi AMCOS kuacha tabia ambayo imeibuka sasa, kwani watakapobainika katika msako huo watachukuliwa hatua kali za kisheria.**

Daudi alisema ofisi yake imepokea malalamiko kutoka kwa wakulima wa pamba kuwa, wapo baadhi ya viongozi wa AMCOS wanauza pembejeo za wakulima kinyume cha maelekezo ya serikali kwani pembejeo hizo zinatolewa kwa mkopo kwa wakulima kupitia vyama vyao vya msingi.

"Niwatake viongozi AMCOS kuacha tabia ambayo imeibuka sasa, kwani watakapobainika katika msako huo watachukuliwa hatua kali za kisheria, na wafanyabiashara walionunua pembejeo hizo kinyume na utaratibu wanapaswa kuzisalimisha kwa Bodi ya Pamba mara moja," alisema Daudi.

Rajabu Masunga, mkulima wa Pamba wilayani Kishapu, aliipongeza Bodi ya Pamba kwa kuwabana wauzaji wa pembejeo za ruzuku zilizotolewa na serikali, ambapo wengi wao walikuwa wakipanga pembejeo hizo chini kwenye minada na kuwauzia wakulima kwa bei ya juu.

Aidha alisema pembejeo hizo kwa Kishapu zimekuwa zikiuzwa kiholela kama kwa kuanikwa juani, na wakulima wengi wamekuwa wakizikosa katika AMCOS zao walizojiunga na kuelekezwa kununua katika minada na magulio, kinyume cha maalekezo ya serikali.

Ashura Juma, alisema kila Alhamisi siku ya mnada wafanyabiashara hupeleka pembejeo (dawa za kuulia wadudu) na kuanza kuwauzia wakulima ambao wamekosa pembejeo hizo kwenye vyama vya msingi na kusababisha pamba ghafu kushuka kila msimu.

Aliishauri Bodi ya Pamba kufika na kufanya ukaguzi Alhamisi, ambayo ni siku ya mnada ili kuhakiki kiwango cha ubora wa dawa zinazouzwa kwa wakulima.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. bilioni 2, juzi toka kwa Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania PLC, Hisham Hendi (kulia) ili kusaidia juhudi za serikali katika kupambana na ugonjwa wa COVID-19 (Corona). Kushoto ni Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa Vodacom Tanzania PLC na Vodacom Foundation, Rosalynn Mworia. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vijiji vyalipa ardhi kiwanda cha sukari

**Na Mwandishi Wetu**

VIJIJI vinane vya wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma, vimetoa hekta 35,000 kwa mwekezaji ili alime miwa na kujenga kiwanda cha sukari.

Hatua hiyo ni juhudi za kutekeleza azma ya serikali ya kuinua uwekezaji nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Simon Anange, alisema hayo wakati akitoa maelezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Geoffrey Mwambe, kwamba kwa vile wananchi wameelewa umuhimu na faida za uwekezaji katika maeneo yaliyokaribu nao, vijiji hivyo vinane vimeamua kutoa sehemu ya ardhi yao ili kuruhusu ulimaji wa miwa, ujenzi wa kiwanda cha sukari na uzalishaji wa malighafi zitakazotumika kiwandani hapo.

Kanali Anange alivitaja vijiji hivyo kuwa ni Nyamidaho, Kumtundu, Nyarugusu, Heru, Ushingo, Kigadye, Kitanga na Kiyugwe na kwamba uwekezaji katika eneo hilo utaratibiwa na TIC.

"Wananchi wenyewe wamehamasishana juu ya umuhimu wa uwekezaji na kutoa uneo kwa halmashauri ili litumike kwa uwekezaji huo. Jambo hili litachochea ukuaji wa kasi wa wilaya yetu," alisema Kanali Anange na kuongeza kwamba kiwanda kikijengwa mapato ya wilaya yataongezeka kwa njia ya kodi, ajira kwa wananchi zitapatikana na kuchochea maendeleo ndani ya wilaya na mkoa kwa ujumla.

"Nawapongeza wananchi wa wilaya hii kwa kujitoa kwao kwa kuachia ardhi kwa hiari kupisha uwekezaji. Jambo hili linaloonyesha kuunga mkono juhudi za Serikali, maana serikali imeazimia kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema Kanali Anange.

Alisema taarifa alizonazo ni kuwa ujenzi wa kiwanda utaanza mwaka huu na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 110,000 za sukari kwa mwaka.

Kiasi hicho cha sukari kitapunguza pengo la upatikanaji wa bidhaa hiyo nchini. Pengo linakadiriwa kuwa takribani tani 320,000 kwa mwaka," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe, alisema wanavijiji wanastahili kupongezwa kwa kuachia eneo lao kwa ajili ya uwekezaji.

"Kituo chetu kitalisimamia eneo hili kikamilifu na kuhakikisha uwekezaji unaofanywa katika eneo hili unawanufaisha wanakijiji wa wilaya ya Kasulu kutokana na kujitoa kwao katika kuunga mkono azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda," alisema Mwambe.

Katika hatua nyingine, TIC ikishirikiana na Kampuni ya Trolle Meesle Limited ya mkoani hapo, wameandaa mafunzo kwa wakulima 1,850 kutoka vyama vinane vya ushirika vinavyolima michikichi mkoani humu.

# Mradi kuongeza upatikanaji maji Moro

WAIZARA ya Maji imesema kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro, itatekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo cha Mto Divue ulipo Turiani katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa kutumia fedha za ndani.

Hayo yalielezwa bungeni jana katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja, ambaye alisema bwawa la maji la Mindu katika Manispaa ya Morogoro limejaa tope na maji hayatoshelezi wananchi wa Manispaa hiyo.

"Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bwawa lingine?"alihoji Minja.

**Mradi huu utatekelezwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Ufaransa (AFD).**

Katika majibu yake, Wizara hiyo ilisema katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji kwenye Manispaa hiyo na kuhakikisha kiwango cha uzalishaji wa maji kinafikia mahitaji kwa asilimia 100, serikali itatekeleza mradi huo.




Ilisema mradi huo utakapokamilika, unakadiriwa kuongeza uzalishaji maji kwa mita za ujazo 27,000 kwa siku.

"Hivyo kufanya jumla ya uzalishaji wa maji katika Manispaa ya Morogoro kuwa mita za ujazo 74,000 kwa siku ikilinganishwa na mahitaji ya sasa ya mita za ujazo 67,086," ilisema.

Aidha, Wizara hiyo ilisema katika mwaka 2020/21, Serikali itapanua mtambo wa kutibu maji wa Mafiga unaotumia chanzo cha bwawa la Mindu ili uweze kuzalisha mita za ujazo 40,000 kwa siku.

"Mradi huu utatekelezwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Ufaransa (AFD)," ilisema.

## Takukuru yaokoa bil. 249/- miaka minne

BUNGE limeelezwa kuwa kwa kipindi cha Disemba 2015 hadi Machi 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(Takukuru), imefanikiwa kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 249.4.

Pia imetaifisha nyumba nane zenye thamani ya Sh. bilioni 11.63, magari matano yenye thamani ya Sh. milioni 126 na viwanja vinne.

Sambamba na hilo, Serikali pia imefanikiwa kuzuia Sh. bilioni 52.8, Dola za Marekani milioni 61.1, magari 14 yenye thamani ya Sh. milioni 635, nyumba 15 zenye thamani ya Sh. bilioni 13.95.

Hayo yalielezwa jana Bungeni na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Mtawara Mjini (CUF), Maftaha Nachuma.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuondoa aina za ufisadi nchini.

Katika majibu ya Ofisi hiyo, ilisema fedha na mali hizo zimepatikana kupitia Kitengo cha Urejeshaji Mali kilichopo chini ya Takukuru ambacho ni maalum kwa ajili ya kurejesha mali zilizopatikana kwa njia za rushwa.

Hata hivyo, ilikiri kuwa serikali ina nia ya dhati ya kuondoa aina zote za ufisadi nchini.

Ilisema kwa dhamira hiyo serikali imeifanyia marekebisho Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 ya Mwaka 2016.

Ilibainisha kuwa, sheria hiyo imefanyiwa marekebisho ya vifungu kadhaa kwa kupanua wigo na kuongeza makosa ya uhujumu uchumi pamoja na kuanzisha Divisheni ya Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu (Mahakama ya Ufisadi na Uhujumu Uchumi) katika Muundo wa Mahakama Kuu.

"Kwa kutambua athari za rushwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini, Serikali imebuni na kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Tatu (NACSAP III) wa Mwaka (2017 - 2022)," ilisema.

Ilieleza kuwa mkakati ni shirikishi na unalenga kuzuia na kupambana na rushwa katika sekta za uchumi za kimkakati zenye mazingira shawishi ya rushwa ambazo ni Manunuzi ya Umma, Ukusanyaji wa Mapato, Uvunaji na Matumizi ya Maliasili, Madini, Nishati, Mafuta na Gesi, Utawala, Vyombo vya Utoaji wa Haki na Shughuli za Vyama vya Siasa.



Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja akichangia moja ya hoja zilizokuwa zikitolewa bungeni. **PICHA: MAKTABA**

## Ataka mikopo elimu isiyo na riba

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Amina Mollel, ameitaka serikali kutoa mikopo isiyo na riba ya elimu ya juu kwa wanafunzi wenye ulemavu.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema watu wenye ulemavu ni miongoni mwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu.

Alieleza kuwa katika kusoma kwao, kuna gharama za ziada za vifaa saidizi hivyo kuwa na mzigo mkubwa wa marejesho tofauti na watu wasio na ulemavu.

"Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati mwafaka kuwapatia watu wenye ulemavu mkopo wa Elimu ya Juu usio na riba?"alihoji.

Pia alihoji serikali haioni umuhimu wa kuwapatia ruzuku ya nyezo za kujimudu badala ya mkopo ili kuwaepushia gharama kubwa ya elimu kutokana na ulemavu wao.

Katika majibu ya swali hilo yaliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilisema mikopo ya Elimu ya Juu inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo (SURA 178).

Ilisema sheria hiyo inabainisha kuwa, mikopo hiyo ni kwa ajili ya wanafunzi wahitaji wenye sifa za kujiunga na Taasisi za Elimu ya Juu.

"Lengo la matakwa haya ya kisheria ni kuwawezesha wanafunzi wote wahitaji wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo wa kiuchumi kupata Elimu ya Juu," ilisema.

Aidha, ilisema wanafunzi wote wenye ulemavu, walioomba na wenye sifa hupatiwa mkopo.

"Mikopo ya Elimu ya Juu inayotolewa na Serikali haitozwi riba kama ilivyo kwa mikopo inayotozwa na taasisi za fedha za kibiashara ambayo ni kati ya asilimia 14 hadi 22, mikopo ya Elimu ya Juu ya Serikali hutozwa asimilia 6 kama tozo ya Kutunza Thamani," ilisema.

Ilifafanua tozo hiyo hukatwa kwenye salio la deni na sio kwenye deni la msingi na katika kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kupata Elimu ya Juu kwa ufanisi, serikali inapeleka fedha za ruzuku kwenye vyuo vikuu kwa ajili ya kununulia vifaa mbalimbali saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Kwa mfano mwaka 2018/19 serikali ilitoa ruzuku ya Sh.Milioni 200 ambazo zilipelekwa vyuo vikuu vinne vya UDSM, UDOM, MUCE na MoCU na mwaka 2019/20 imetenga Sh.Milioni 250," ilisema.

Aidha, ilisema serikali inatoa ruzuku kwenye vyuo vikuu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Nipashe
TESA
Jumanne Aprili 21, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 13



Kuruhusu vitabu bila ithibati ni kuua elimu

MABINTI HATARINI

## NA SABATO KASIKA

# Likizo ya corona yawa msimu wa ukeketaji

UKIWA ni mkakati wa mwanzo kuzuia kusambaa kwa maambukizi ya virusi vya corona(COVID 19) kupitia mikusanyiko, Machi 17, mwaka huu, serikali ilitangaza kufunga shule za msingi, sekondari na vyuo vyote kwa muda wa mwezi mmoja.

Wakati inafunga shule, msisitizo kwa wanafunzi ni kutulia nyumbani kwao ili muda huo wa likizo ya dharura usipite bure huku ikiwataka wazazi kutoruhusu watoto wao kuzurura au kwenda kusalimia ndugu, jamaa na marafiki kwani lengo ni kuwabakiza nyumbani na kuwakinga na ugonjwa.

Hata hivyo, baadhi ya wazazi na walezi badala ya kuhimiza watoto wasome, wameamua kuwapeleka mabinti kwa ngariba wakakeketwe.

Haya yanabainishwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Daniel Shillah, katika mazungumzo yake na gazeti hili, kwamba wapo baadhi ya wazazi mkoani kwake wametumia likizo hii kukeketa watoto wao.

Shillah anathibitisha kuwapo kwa tukio la kupatikana kwa wasichana hao baada ya kufanya msako wa nyumba kwa nyumba ya kuwasaka wazazi wa aina hiyo kwenye baadhi ya vijiji vya wilaya ya Serengeti na kunasa watoto 19 huku watano kati yao wakiwa wameshakeketwa.

"Tulipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kuhusu kuwapo kwa vitendo vya ukeketaji, tukafuatilia na kupata watoto hao, huku wengine wakiwa tayari wameshakeketwa,"anasema Kamanda Shillah.

Anaeleza kuwa polisi inashirikiana na wadau mbalimbali likiwamo shirika la Kutetea Haki za Wanawake, Wasichana na Watoto la Hope for Girls and Women Tanzania.

"Hao ndiyo waliotoa taarifa na kufanikisha kupata idadi hiyo ya wasichana ambao wengi wao ni wanafunzi, na kwa sasa wanatunzwa katika nyumba salama ya shirika hilo iliyopo mjini Mugumu," anasema.

Aidha, anawataka wazazi kutambua kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria na kwamba wahusika wakikamatwa watawafikisha mahakamani kwa kosa la jinai, na kuwataka wenye mtindo huo waache.

"Wahusika wamekimbia, lakini tunaendelea kuwafuatilia ili sheria ichukue mkondo wake, lakini pia ipo haja ya kutoa elimu zaidi kwa wazazi ambao bado wanaendelea kukumbatia mila hizo potofu waachane nazo," anasema.

Kamanda Shillah anasema, vita dhidi ya ukeketaji haiwezi kumalizwa na polisi kwa kutumia bunduki bali ni elimu kwa jamii kama ambayo imekuwa ikitolewa na Hope For Girls and Women Tanzania.



Baadhi ya wasichana wanaokimbia ukeketaji na kulelewa katika kituo cha nyumba salama ya Mugumu, wakifanya usafi kwenye barabada inayoelekea kituoni hapo.. **PICHA: MTANDAO**

> Tulipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kuhusu kuwapo kwa vitendo vya ukeketaji, tukafuatilia na kupata watoto hao, huku wengine wakiwa tayari wameshakeketwa

### OPERESHENI USAKAJI

Mkurugenzi Mtendaji wa Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samweli, anasema, shirika lake linatoa taarifa za ukeketaji ndani ya jamii, ambapo walilifahamisha kuwapo kwa vitendo hivyo.

"Baada ya kupata taarifa ilifikishwa dawati la jinsia la polisi hapa kwetu Mugumu ndipo tukaenda kufanya operesheni ya kuokoa wasichana wasikeketwe," anasema Rhobi.

Anaeleza lkuwa operesheni hiyo ilifanyika kwa muda wa siku saba kuanzia Aprili mosi hadi 7 katika vijiji vya Machochwe, Burunga, Kebencha, Nyansurura, Matare na Kenokwe, wakafanikiwa kupata idadi hiyo ya wasichana.

Anasema, wasichana hao akiwamo mtoto wa kiume aliyechukuliwa baada ya kukuta akifanyiwa mateso makali na wazazi wake, wapo katika kituo cha nyumba salama cha Mugumu huku hatua nyingine zikifuata.

"Mojawapo ya hatua hizo ni kwenda kwa wazazi ili kujenga uhusiano mwema na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukeketaji na wakikubali, kubadilika tutawaruhusu wawachukue watoto wao," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, kama alivyo mtoto wa kiume, hata wa kike naye anatakiwa aachwe asome badala ya kumkeketa kwa ajili ya kumuandaa kuolewa ili wazazi wapate mali.

Rhobi anasema, kwa kawaida ukeketaji hufanyika Desemba, lakini wameamua kutumia likizo ya corona kufanya ukatili huo, kwa vile wanajua kuwa mwezi huo hata vyombo vya dola vinaujua kuwa ni wa ukeketaji, hivyo watadhibitiwa.



Vifaa ambavyo hutumiwa na ngariba kufanya ukatili huo dhidi ya watoto wa kike.

### KUFUATILIWA ZAIDI

Kwa upande wake Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mara, Ephraem Simbeye, anasema amesikitishwa na taarifa hizo za baadhi ya wazazi kutumia likizo hiyo kukeketa watoto wao.

Anasema, mila hizo siyo za kukumbatia, kwa sababu zina madhara kiafya na pia zinakwamisha maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike, hivyo wanaozikumbatia wanatakiwa kushurutishwa kuziacha.

"Serikali imefunga shule kutokana na tishio la corona ili watoto wakae nyumbani wajisomee, sasa inashangaza kusikia kuna wazazi wameamua kutumia nafasi hiyo kuharibiwa watoto wao ratiba," anasema Simbeye.

Anasema, atawasiliana na wasaidizi wake katika wilaya zote zenye mtindo wa kukeketa ili wasaidiane na wa chini yao kutafuta taarifa za kuwapo kwa vitendo hivyo na kuzifikisha kwenye vyombo vya dola.

### MADHARA

Mganga Mkuu wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti, Dk. Tanu Waryoba anathibitisha kupokea watoto waliofanyiwa ukeketaji na kuwachunguza na kubaini kuwapo kwa tukio hilo na kuonya kuwa ukeketaji una madhara ikiwamo maambukizi ya magonjwa kwa vile hufanywa kwa kuchangia vifaa na wakati mwingine husababisha vifo kwa kutokwa damu nyingi.

# POLISI KATIKA MPAKA WA TANZANIA NA MSUMBIJI

**MWEZI mmoja uliopita, kumekuwapo na sintofahamu katika mji wa Mocimboa da Praia, ulio kaskazini mwa jimbo la Cabo Delgado, ambapo raia, kikosi cha jeshi na vituo vya polisi vilishambuliwa.**

Washambuliaji hao wanadaiwa kuharibu nyumba za wananchi, mali za umma na kuweka vizuizi barabarani na kutishia amani baada ya kuteka kambi ya jeshi na kituo cha polisi na kusababisha wanavijiji wengi kukimbia makazi yao.

Sintofahamu hiyo inaiweka Tanzania katika hali ya tahadhari na hivi karibu Jeshi la Polisi limeweka ulinzi madhubuti katika eneo hilo ambalo linapakana na Tanzania kwenye mkoa wa Ruvuma.

Jeshi la Polisi limeendelea kukagua njia za panya zinazotumiwa na raia mbalimbali kuja nchini na ambazo pia huweza kutumiwa na maadui wanaofanya mashambulizi kwenye eneo hilo lililo kaskazini mwa Msumbiji



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas, akizungumza na Mzee Abdul, mkazi wa Kijiji cha Ndondo wilayani Nyasa mkoani Ruvuma, wakati akiendelea na operesheni ya ukaguzi wa mpaka.. **PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI.**



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi La Polisi, Sabas, na Mkuu wa Operesheni Maalum za Jeshi la Polisi, Mihayo Msikhela pamoja na maofisa, wakaguzi na askari wakikagua njia inayotumiwa na wananchi wa Msumbiji kuingia nchini bila ya kuwa na vibali maalum.



Kamishna wa Jeshi la Polisi wa Mafunzo na Operesheni, Liberatus Sabas, akiendelea na operesheni ya kukagua mpaka wa Tanzania na Msumbiji hasa katika vipenyo na njia zisizo rasmi wanazotumia wananchi wa Msumbiji kuingia Tanzania kinyemela.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA

# Kuruhusu vitabu bila ithibati ni kuua elimu

VITABU ni nyenzo muhimu ya kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji bora. Maarifa yatolewayo katika taasisi mbalimbali za elimu na sehemu nyinginezo, yamehifadhiwa vyema katika vitabu vilivyoandaliwa na waandishi mbalimbali. Walimu na wanafunzi kwa pamoja husoma vitabu ili kupata maarifa. Vipo vitabu vya kiada na vitabu ya ziada ambavyo kwa pamoja hutumika katika kuchagiza ufundishaji na ujifunzaji wenye mawanda mapana ya maarifa.

Kutokana na umuhimu wa vitabu katika ufundishaji na ujifunzaji, ni lazima vinavyotumika viwe ni vile vyenye ithibati tu ili kuwa na uelewa wa pamoja kwa walimu na wanafunzi. Ithibati ni muhuri unaodhihirisha ukweli, kwa ufupi ni uthibitisho.

Lipo wimbi la waandishi wengi wa vitabu vya ziada ambavyo hazijapata ithibati ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ambayo imepewa mamlaka ya kupitia, kuchambua na kutoa ithibati ya vitabu vya kiada na ziada ili viweze kutumika katika kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari Tanzania.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, anatoa agizo kwa serikali kuhakikisha kuwa shule za serikali na zile za binafsi zinatumia vitabu vya kiada na ziada vyenye ithibati katika kufundishia na kujifunzia ili kuwezesha maudhui ya elimu wanayopata wanafunzi yanakuwa bora na kukidhi vigezo.

Taasisi ya Elimu Tanzania inatoa ithibati kwa vitabu vilivyokidhi ubora na vigezo tu. Hivyo basi, kama vitabu vitatumika bila kuthibitishwa, upo uwezekano mkubwa wa wanafunzi kufundishwa masuala mbalimbali nje na malengo na matarajio yaliyowekwa.

Katika hafla ya uzinduzi wa kazi ya kusambaza vitabu vya kiada kwa shule za msingi zinazotumia Kiingereza katika kufundishia na vitabu vya nukta nundu kwa darasa la I-V na kidato cha nne, Waziri Nasha anasema "Vitabu hivi ndiyo moyo wa elimu, hivyo walimu na wanafunzi wanapaswa kuvitumia wakati wa kufundisha na pia wanafunzi wavitumie kwa kujifunza na si kuviweka stoo".

Vitabu hivyo ni vile ambayo zimepata ithibati ya Taasisi ya Elimu ambavyo vinakidhi mahitaji na vigezo kwa ajili ya kutumika kufundishia na kujifunzia shuleni.

Kwa kuwa vitabu ni moyo wa elimu, haipaswi kuwa na uholela wa kutumia kitabu chochote kufundisha wanafunzi. Taasisi ya Elimu inatambua uwepo wa waandishi binafsi katika kusaidia maendeleo ya elimu kupitia maandishi yao, lakini hawapaswi kuchapisha vitabu na kuviingiza katika mzunguko bila vitabu hivyo kupata ithibati ya Taasisi ya Elimu kwa ajili ya kuanza kutumiwa na walimu na wanafunzi.

> “Vitabu hivi ndiyo moyo wa elimu, hivyo walimu na wanafunzi wanapaswa kuvitumia wakati wa kufundisha na pia wanafunzi wavitumie kwa kujifunza na si kuviweka stoo

Vitabu visivyo na ithibati ni sumu, vikitumika vitasababisha kuua elimu ambayo serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo wametumia gharama kubwa kuinua na kuikuza. Waandishi watangulize maslahi ya taifa kwa kuhakikisha vitabu wanavyoandika vimepitia hatua zote muhimu badala ya kuandika vitabu kwa lengo la kufanya biashara bila kuzingatia athari watakayopata walaji yaani walimu na wanafunzi.

Vitabu vya ziada vyenye lengo la kuongeza maarifa kwa walimu na wanafunzi baada ya kusoma vitabu vya kiada, ni lazima vikidhi vigezo vya kulandana na vitabu vya kiada ili kumsaidia msomaji kuongeza maarifa ya ziada anayoyatafuta.

Kwa waandishi ambao wanataka vitabu vyao vitumike kama vitabu vya kiada na ziada wahakikishe kuwa wanawasilisha kazi zao kwenye mamlaka za Taasisi ya Elimu, ili kupata ithibati ili vitabu hivyo kuvipa uhalali wa kisheria wa kutumika katika maendeleo ya elimu.

Waandishi wasione kuwa kufanya hivyo ni usumbufu bali ni utaratibu uliowekwa kuhakikisha nchi yetu inasimamia kikamilifu sekta ya elimu ambayo ndiyo sekta mama ya kuchangia maendeleo katika sekta nyingine zote. Uholela wa vitabu unazaa elimu duni isiyokidhi vigezo vya kuwa na wasomi waliondaliwa vyema kumudu ushindani katika soko la ajira.

Endapo kazi ya mwandishi itakosolewa kwa kutokukidhi viwango na vigezo, mwandishi azifanyie kazi kasoro zitakazokuwa zimetolewa na mamlaka ili kuboresha kazi yake ili iwe bora zaidi inayofaa kutumika nchi nzima. Tukiwa katika harakati za kuifanya nchi yetu kuwa ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, ni lazima kudhibiti vitabu visivyokidhi vigezo vilivyoainishwa.

Tukifanikiwa kuwa na vitabu bora, vyenye viwango vya kitaifa na kimataifa, tutakuwa na wasomi bora, wenye maarifa yanayoendana na mahitaji ya sasa. Kwa wanunuzi wa vitabu, wanao wajibu wa kukagua ithibati kwa vitabu wanavyotaka kununua ili kujiridhisha na ubora wa vitabu hivyo. Kwa vitabu ambayo havitakuwa na ithibati, wanunuzi wasivinunue kwani ni sumu inayoweza kuua elimu yetu. Kwa pamoja tuseme hapana vitabu visivyo na ithibati. Tafakari.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0764 -666349.***




Wanafunzi wakiulizia na kununua vitabu kwenye maonyesho mbalimbali ya kusoma na kujifunza. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Corona kuimaliza Afrika kiuchumi

● Ifikirie kuunda fuko la kujinusuru

MAGWIJI wa uchumi duniani wanasema virusi vya COVID-19 vitaporomosha uchumi wa nchi za Afrika zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa asilimia 1.6.

Ni takwimu zinazotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), likitaja mambo kadhaa muhimu ya kuzingatiwa ili kupunguza madhara ya kibinadamu na kiuchumi yatokanayo na janga la ugonjwa wa virusi vya corona.

COVID-19 kwa nchi za Afrika zilizo kusini ya Sahara, IMF inasema katika ripoti yake ya wiki iliyopita iliyotolewa jijini Washington DC kuhusu mtazamo wa shirika hilo kwa uchumi wa mataifa hayo wakati huu ambapo shirika hilo limesema janga la corona litasababisha uchumi wa mataifa hayo ya Afrika kusinyaa kwa asilimia 1.6.

Asilimia 1.6 za kudorora uchumi huo ni kiwango cha juu zaidi cha mporomoko wa uchumi kuwahi kurekodiwa na kwamba si habari njema.

"Janga hili litafuta maendeleo ya hivi karibuni kwenye ukanda wote na hata kwa miaka ijayo," amenukuliwa Abebe Aemro Selassie, Mkurugenzi wa Idara ya Afrika wa IMF.

Anasema kuwa viashiria vyote ni kwamba, "COVID-19 itakuwa na madhara makubwa ya kibinadamu na kiuchumi, uchumi wa dunia ukiyumba, udhibiti wa fedha ukiongezeka, bei za bidhaa zinazouzwa nje zikiporomoka na kutibuka kwa shughuli za kiuchumi kutokana na hatua za kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona."

Mathalani, Selassie, anasema vipato vya watu vimeporomoka na hivyo kuongeza pengo la ukosefu wa usawa, hatua za watu kutochangamana kuzuia watu wengi kushindwa kupata kipato chao.




Kunawa mara kwa mara na maji safi na sabuni ni moja ya njii kuu za udhibiti wa corona zinazosisitizwa. Lakini, kunawa huku kunakokusanya maji kwenye madumu ambayo ni vigumu kuyabeba ili kumwaga majitaka serikali imekutolea muongozo gani? **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

### ILI KUNUSURU

Ni kwa mantiki hiyo mkuu huyo wa Idara ya Afrika ya IMF ametaja hatua muhimu tatu ambazo amesema ni muhimu ili kudhibiti gharama za kiuchumi zitokanazo na COVID-19.

Hatua ya kwanza ni kutoa kipaumbele ili kuongeza fedha kwenye sekta ya afya ya umma ili kudhibiti mlipuko bila kujali bajeti ya nchi. Pili ni kuhakikisha kuwa msaada mkubwa na unatolewa wakati muafaka akisema kuwa, sera zinapaswa kujumuisha uhamishaji wa fedha au msaada wa vitu kwa kaya maskini wakiwamo wafanyakazi vibarua. Msaada pia ulenge sekta zilizodhurika zaidi. Uwezo wa nchi kupata fedha unategemea kwa kiasi kikubwa uwezo wao wa kupata fungu la msaada kutoka jamii ya kimataifa."

Aidha, Selassie, Anataja hatua ya tatu kuwa ni será za fedha lazima ziwe na dhima muhimu katika kuendeleza kampuni na ajira.

Mkuu huyo wa Idara ya Afrika, IMF anaeleza kuwa katika kusaidia hatua za ndani, hatua zinazoratibiwa na wadau wote wa maendeleo ni muhimu.

> "COVID-19 itakuwa na madhara makubwa ya kibinadamu na kiuchumi, uchumi wa dunia ukiyumba, udhibiti wa fedha ukiongezeka, bei za bidhaa zinazouzwa nje zikiporomoka na kutibuka kwa shughuli za kiuchumi kutokana na hatua za kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona.

Anasema IMF inashirikiana na wadau hao ambao ni Benki ya Dunia, shirika la afya la Umoja wa Mataifa (WHO), Benki ya Maendeleo Afrika na Muungano wa Afrika (AU) ili kukabili haraka janga la COVID-19.

Selassie anaeleza kuwa IMF imejiandaa kutoa Dola bilioni 11 kwa nchi 32 za Afrika zilizo Kusini mwa Sahara ambazo ziliomba msaada wiki za karibuni na tayari baadhi yao zimeshapata zikiwamo, Burkina Faso, Chad, Gabon, Ghana, Madagascar, Niger, Rwanda, Senegal, na Togo.

Anaeleza kuwa fedha hizo kwa nchi maskini zaidi na zilizo hatarini zaidi ni kutoka katika mfuko wa IMF wa kudhibiti majanga akisema wakati huu shirika hilo linahitajika zaidi na wanachama ili kuweza kupunguza mzigo wa gharama kwenye sekta ya afya.

### JITIHADA ZA NDANI

Pamoja na changamoto ya corona na Umoja wa Afrika (AU) kushirikiana na IMF, ni wazi Waafrika wameona jinsi dunia au kila taifa au ukanda ulivyosimama wenyewe kujitetea dhidi ya corona.

Mfano takribani Yuro bilioni 500 zimetolewa na mataifa ya Umoja wa Ulaya kusaidia kunusuru uchumi wa nchi wanachama.

Wawakilishi wa mataifa 19 ya ukanda wa sarafu ya Yuro wamekubaliana kutolewa mara moja kiasi cha Euro bilioni 500 kwa ajili ya kuuimarisha uchumi wa Ulaya.

Hatua hiyo imefikiwa wakati ikipambana kunusuru kuanguka kwa uchumi kutokana na janga la corona.

Waziri wa fedha wa Ufaransa, Bruno La Maire, anasema makubaliano hayo ni mazuri mno. Mataifa makubwa kiuchumi Ulaya, Ujerumani na Ufaransa yamekuwa yakipambana kupata suluhu ya kushughulikia athari za kiuchumi kufuatia janga hilo, wakati mawaziri wa fedha wakijadiliana kuhusu suala hilo jana Alhamisi.

Waziri wa Fedha wa Ujerumani, Olaf Scholz, amesifu uamuzi huo akitaja kama siku njema kwa mshikamano wa Ulaya.

Afrika imejifunza kuwa nayo sasa inatakiwa kuwa na fuko wa kushughulikia maafa. Matatizo kama hayo yanatakiwa kushughulikiwa na AU kupitia chombo kama hicho cha Umoja wa Ulaya.\

Benki ya Maendeleo ya Afrika 'the African Development Bank' licha ya kutangaza mikakati ya kujilinda na kuepusha wafanyakazi wake na corona, haijawa taasisi madhubuti ya kukabiliana na hali tete ya uchumi , kuna haja ya kuamka na kuangalia namna ya kujinusuru na tatizo la uchumi kudorora na kusaidia kampuni na viwanda vya Afrika kuzalisha .



# Wataalamu wahofia corona kuleta njaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATAALAMU wa utafiti za mbegu bora za kilimo nchini, wametahadharisha kuwa kuenea kwa kasi kwa virusi vya corona huenda kukaathiri utafiti wa kilimo Tanzania, hali ambayo itasababisha njaa na umaskini.

Walisema kwamba endapo wakulima watazuiliwa kushiriki katika utafiti mbalimbali unaoendelea kutokana na maambukizi ya corona, kuna uwezekano mkubwa wa kuathiri shughuli za utafiti ikiwamo upatikana wa mazao bora mashambani.

Akizungumza na Nipashe, Mtafiti na Mzalishaji Mkuu wa mbegu katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kituo cha Hombolo, Dk. Lameck Nyaligwa, alisema kuna haja kubwa ya Serikali kuwaruhusu wataalamu wa utafiti wa mbegu bora za mazao kuendelea na shughuli zao za kitafiti ambazo zinahitaji mjumuiiko mkubwa wa wakulima husika.

Dk. Nyaligwa alitoa wito huo kutokana na katazo la serikali la mkusanyiko wa watu wengi katika maeneo mbalimbali, zikiwa ni juhudi za kupunguza kasi ya maambizi ya orona.

"Utafiti wa mbegu kwa kiasi kikubwa unahitaji ushirika wa wakulima husika, wakati mwigine zaidi ya wakulima 100, hivyo tunaiomba Serikali kufikiria jambo hili," alisema.

Aliongeza kuwa sekta ya kilimo imeajiri takribani asilimia 80 ya Watanzania, na inachangia asilimia 30 ya pato la taifa, huvyo ni muhimu kwa watafiti sekta hiyo muhimu waendelee na utafiti wao.

"Kwa mfano, TARI-Hombolo tangu mwaka jana imeanza kutekeleza utafiti mbalimbali wa mbegu bora za mazao ya mtama, alizeti na uwele kwa ushikiano na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi... miradi ya gharama kubwa na yenye umuhimu mkubwa katika kuendelezaji sekta ya kilimo nchini," aliongeza.

Aidha, alisema, miradi hiyo ambayo kwa sasa inatekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini, inahitaji wataalamu husika kusafiri na kukutana na wakulima ili kuwezesha mbegu hizo zilizo katika majaribio kuthibitishwa na Mamlaka ya Taifa ya Kuthibisha ubora wa Mbegu (Tosci).

# Ewura: Bei ya mafuta kutopanda kwa sasa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imesema bei ya mafuta nchini haitaongezeka kutokana na athari za kiuchumi zinazoendelea duniani kutokana na kuenea kwa kasi kwa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na hofu kubwa miongoni mwa watumiaji wa nishati ya mafuta juu ya uwezekano wa bei kuongezeka kutokana na athari za kiuchumi duniani zinazotokana na kueneza kwa kasi ugonjwa huo.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Meneja wa Mahusiano na Mawasiliano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema kinyume cha matarajio ya wengi, bei za mafuta nchini zinatarajia kuendelea kushuka kutokana na kupungua kwa kasi kwa mahitaji ya nishati za mafuta katika soko la dunia.

**Tunatarajia kupokea tani nyingine nyingi za mafuta ambazo zitaanza kutumika mwezi wa sita, kwani kwa sasa mafuta tuliyoingiza miezi miwili iliyopita yanaendelea kutumika.**

"Shughuli nyingi zinazotegemea nishati ya mafuta duniani zimefungwa na kusitishwa, hali ambayo imepelekea mdororo wa uhitaji wa nishati za mafuta duniani na Tanzania pia. Hali hii kwa upande mwingine, imeleta unafuu mkubwa kwa watumiaji wa mafuta kwa sababu bei za mafuta huenda zikaendelea kushuka," alisema.

Kaguo alisema Tanzania ina akiba ya kutosha ya kukidhi mahitaji ya matumizi ya mafuta kwa sasa na kuongeza: " Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta, tunatakiwa kuwa na akiba ya angalau siku 15 za ziada za mafuta, hata hivyo, kwa sasa tuna akiba ya kukidhi mahitaji ya mafuta ya miezi miwili ijayo."

Aidha, alisema uagizaji wa mafuta nchini kwa sasa unaendelea kama kawaida, na kwamba mwishoni mwa mwezi jana, tani nyingine nyingi za mafuta ziliwasili nchini kwa ajili ya matumizi ya miezi miwili ijayo.

"Tunatarajia kupokea tani nyingine nyingi za mafuta ambazo zitaanza kutumika mwezi wa sita, kwani kwa sasa mafuta tuliyoingiza miezi miwili iliyopita yanaendelea kutumika," alisema Kaguo.

Alisema kwa sasa, mahitaji ya nishati ya mafuta kwa mwezi kwa Tanzania ni takribani tani 300,000, na kwamba mamlaka inaendelea na jitihada mbalimbali ya kuhakikisha nishati hiyo muhimu inapatikana kwa urahisi na kwa bei elekezi katika maeneo yote nchini.

"Kwa sasa tunatekelea mkakati maalumu wa kufungua vituo ya mafuta vinavyotembea (mobile fuel stations) katika maeneo ya vijijini ili kuhakikisha Watanzania wanaokaa maeeo hayo wananufaika na huduma za mafuta," alisema.

Mkakati huo, alisema unalenga kupunguza wimbi la uuzwaji na uhifadhi holela wa mafuta vijijini, hali ambayo mara nyingi imekuwa ikisababisha maafa ya majanga ya milipuko ya moto.




Wafanyabiashara wa mboga, wakifanya biashara zao katika mazingira hatarishi kwa afya ya mlaji kutokana na kuziweka ardhini, katika Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Askofu ataka bajeti ya dharura corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Maombezi (Endles time Harvest), Dk. Eliah Mauza, amewataka wabunge kabla Bunge la bajeti halijafikia mwisho, wapendekeze serikali ipeleke hati ya dharura bungeni ili Wizara ya Afya, iongezewe fedha katika bajeti yake itakayosaidia kuendesha zoezi la upimaji wa maambukizi ya virusi vya corona nyumba kwa nyumba.

Hivi karibuni, Rais kupitia ukurasa wake wa Twitter aliandika: "Ndugu zangu Watanzania kutokana na ugonjwa wa corona nawaomba tutumie siku tatu za kuanzia Aprili 17 hadi 19, 2020, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili kumuomba Mwenyezi Mungu aliyemuweza wa yote kutuepusha na janga la ugonjwa huu, tusali kila mmoja kwa imani yake atatusikia."

Kutokana na maombi hayo juzi, ikiwa ni siku ya mwisho ya maombi hayo ya siku tatu, Askofu Mauza aliongoza waumini wa kanisa hilo kuliombea Taifa juu ya ugonjwa huo.

Askofu Mauza, aliwaomba wabunge waishauri serikali kupeleka hati ya dharura bungeni ili Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto kupatiwa fedha ili ifanye upimaji wa maambukizi ya virusi vya corona mlango kwa mlango.

Alisema upimaji wa nyumba kwa nyumba utawezesha Watanzania wengi kujua afya zao, hivyo kupunguza idadi ya maambukizi ambayo inaendelea kupanda kwa kasi.

"Hili jambo ni la dharura, hivyo ni lazima hata watendaji wa Serikali ikiwezekana waandae hati ya dharura ambayo itasaidia Wizara ya Afya kuongezewa fedha ambazo zitasaidia zoezi la upimaji mlango kwa mlango na kutambua wenye maambukizi ya virusi vya corona," alisema.

"Kama wakati wa Mwalimu Nyerere, ilipotokea dharura ya vita vya Iddi Amin, kila mmoja alifundishwa jinsi ya kutumia silaha na kwenda kuongeza nguvu katika mapambano yale, hivyo hata sasa haya ni mapambano, lazima tuhakikishe kila mtu kwa nafasi yake anashiriki katika vita hivi vya kupamba na janga hili linaloitikisa dunia," alisema.

Alisema anampongeza Rais Magufuli, kwa kuona kuna umuhimu wa kutangaza siku tatu za maombi ambapo alishauri kwamba anaweza kuongeza siku zingine saba au 21 ili waweze kuomba zaidi.



# Shule yakarabatiwa baada ya miaka 58

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umeamua kutumia kipindi hiki ambacho shule zote zimefungwa kwa ajili ya tahadhari ya ugonjwa wa corona kufanya ukarabati mkubwa wa shule ya Sekondari ya kutwa ya Mbeya (Mbeya Day), ambayo baadhi ya majengo yake yamechakaa na kuhatarisha usalama wa wanafunzi.

Shule hiyo ilijengwa mwaka 1962, mwaka mmoja baada ya nchi kupata Uhuru, lakini haijawahi kufanyiwa ukarabati, hivyo baadhi ya majengo yana hali mbaya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye aliongozana na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo kukagua ukarabati wa shule hiyo, alisema waliamua kufanya ukarabati huo kipindi ambacho shule zimefungwa kwa sababu hakuna pilikapilika za wanafunzi.

Alisema ukarabati huo unafanywa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kikosi namba 844 KJ Itende cha jijini Mbeya kwa gharama ya Sh. milioni 142 na kwamba kwa sasa kikosi hicho kwa kushirikiana na kamati ya ujenzi ya shule hiyo kimetumia Sh. milioni 50 kununua vifaa.

**Kukarabatiwa kwa majengo ya shule hiyo kutapelekea kuwa na mazingira mazuri ya kazi kwa walimu na wanafunzi kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia.**

"Shule zimefungwa lakini Serikali haijaacha kuleta fedha kwa ajili ya maendeleo na ndio maana sisi hapa tumeletewa na Mheshimiwa Rais Sh. milioni 795 kwa ajili ya ukarabati wa shule yetu, lengo letu ni kuifanya shule hii kuwa kioo chetu," alisema Chalamila.

Alisema matatizo yanayoikabili shule hiyo ni uchakavu wa miundombinu, lakini ina walimu wa kutosha pamoja na wanafunzi na kwamba ukarabati ukikamilika itakuwa miongoni mwa shule bora zinazomilikiwa na Serikali.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusula, alisema wameamua kutumia maafande wa JKT kukarabati shule hiyo kwa lengo la kuharakisha kazi hiyo ili shule zitakapokuwa zinafunguliwa wanafunzi wakute kazi imekamilika.

Alisema vijana hao wamefanya kazi kwa siku nne, lakini kazi waliyoifanya inaonekana kama ni ya miezi mitatu na kwamba hali hiyo inaleta matumaini kuwa watakamilisha mapema.

Alisema Halmashauri hiyo ina uzoefu wa kuwatumia maafande hao kwenye ujenzi na ukarabati wa shule na ndio maana hawana shaka lolote kuhusu ubora wa kazi inayoendelea katika shule hiyo.

"Tunaamini kuwa, hawa wenzetu watakamilisha kazi hii kwa muda tuliokubaliana na watakamilisha kwa ubora, tumeshawatumia kwenye ukarabati wa Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Azimio na tunawatumia pia kujenga shule kule Airport," alisema Kasusura.

Alisema Serikali itahakikisha inawapa ushirikiano maafande hao ili kusiwe na mkwamo wa aina yoyote kwenye mradi huo na kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha muda huu ambao shule zimefungwa unatumika vizuri.

Mkuu wa shule, Mwalimu Magreth Haule, alisema shule hiyo imechakaa kutokana na kuwa na umri mkubwa na hivyo anaishukuru Serikali kwa kuamua kuikarabati.

Alisema kukarabatiwa kwa majengo ya shule hiyo kutapelekea kuwa na mazingira mazuri ya kazi kwa walimu na wanafunzi kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia.

# Upulizaji dawa kwenye mabasi waanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya, limeanza kupulizia dawa ya kuua virusi vya corona kwenye mabasi yote yanayoanzia safari zake jijini humo kuelekea maeneo mbalimbali.

Ofisa Afya wa Jiji la Mbeya, Johnson Ndaro, alisema walianza utaratibu huo kwa kuanza na mabasi ya kwenda katika mikoa mbalimbali ambapo wanatumia kemikali aina ya Chlorine ambayo wanapuliza kwenye mabasi yote kabla abiria hawajaingia.

Alisema baadaye wataanza kwenye magari madogo ya abiria yanayofanya safari zake katikati ya jiji hilo (daladala) pamoja na pikipiki za magurudumu matatu (bajaji ili kuhakikisha ugonjwa huo hauenei.

"Tunapuliza dawa hii gari zikishusha abiria ili wengine watakapokuwa wanaingia wasiambukizwe kama pengine waliokuwa wamepanda wana maambukizi, zoezi hili litakuwa endelevu," alisema Ndaro.

Alisema shughuli hiyo wanaifanya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na wamiliki wa mabasi ili kuhakikisha linafanyika kwa ufasaha na kila gari linapuliziwa.

Hata hivyo, alisema Mkoa wa Mbeya haujaripoti kisa chochote cha ugonjwa huo, lakini wameamua kuchukua tahadhari kutokana na muingiliano wa watu kutoka maeneo mbalimbali ya nchi.



Mkazi wa Kijiji cha Igoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, akiwa amejitwisha mzigo wa kuni kwa ajili ya nishati ya kupikia, akirejea nyumbani kutoka msituni, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ankara kubwa maji Mbeya-WSSA zalalamikiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakazi wa Jiji la Mbeya, wameilalamikia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), wakidai kuwa inawabambikia Ankara kubwa za maji hali ambayo inasababisha washindwe kulipia huduma hiyo.

Wakizungumza na wandishi wa habari kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema kumekuwa na ongezeko la gharama za huduma hiyo lisilokuwa la kawaida katika kipindi cha miezi mitano kuanzia Novemba mwaka jana mpaka Machi mwaka huu.

Tully Nelson, alisema aliunganishiwa huduma hiyo nyumbani kwake mwaka 2013, na kwamba matumizi yake ni ya kawaida ambayo awali alikuwa analipa kati ya Sh. 3,000 na 15,000 kwa mwezi kulingana na matumizi.

Alisema alikuwa analipa gharama hizo baada ya Mamlaka hiyo kumtumia gharama za matumizi, lakini kuanzia Oktoba na Novemba mwaka jana hakutumiwa ujumbe wowote mpaka alipoamua kuwapigia simu mwenyewe.

Alisema baada ya kuwapigia simu ndipo walipomtumia ujumbe unaoonyesha kuwa alikuwa anadaiwa Sh. 95,000, gharama ambayo alidai ni tofauti na matumizi yake halisi.

"Hawa wameamua kuanza kututesa, hizi gharama zinatufanya sasa tushindwe kulipia huduma yao na kuna uwezekano wakaja kutukatia maji majumbani, tunaiomba Serikali ifanye uchunguzi," alisema Tully.

Naye, Lusajo Mwakifwamba, alisema mamlaka hiyo imekuwa ikimtumia ankara ambazo zinabadilika mara kwa mara bila sababu yoyote, hali ambayo inamfanya awe na wasiwasi na utendaji wa watumishi wa mamlaka hiyo.

Alisema Januari aliletewa ankara ambayo ilikuwa inaonyesha alikuwa anadaiwa Sh. 16,000, lakini ghafla mwezi Februari aliletewa aknara inayoonyesha kuwa alitakiwa kulipa Sh. 175,000 na Machi akaletewa ankara ambayo inaonyesha anatakiwa kulipa Sh. 12,000.

"Sasa tunashindwa kuelewa tatizo ni nini, mimi matumizi yangu ni ya kawaida sana na hizo gharama za Januari na Machi sina tatizo nazo, lakini hii ya Februari sio matumizi yangu na nitashindwa kuilipa," alisema Mwakifwamba.

Alpher Mushi, alisema baadhi ya wananchi kwenye maeneo ya jiji hilo walishasitishiwa huduma ya maji na Mbeya-WSSA, lakini bado wanapelekewa ankara kubwa wakitakiwa kulipa.





# Ajisalimisha kwa DC maelezo kukwama mradi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Kampuni ya Grative Tanzania Limited yenye makao makuu Dar es Salaam, ametekeleza agizo la Mkuu wa Wilaya Kaskazini B, Rajab Ali Rajab, la kumtaka aripoti ofisini kwake Aprili 17, asubuhi kutoa maelezo ya kuhusiana na kuchelewa kumalizika kwa wakati mradi wa ujenzi wa tangi la kuhifadhia majisafi na salama linalojengwa katika Kijiji cha Kitope.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B, Rajab Ali Rajab, kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Aprili 4, kufuatia kuchelewa kukamilika kwa wakati mradi huo uliopangiwa kumalizika Desemba mwaka jana, licha ya kuongezewa muda wa miezi mitatu bila ya kufikia lengo.

**Mkandarasi wa mradi huo alizuiliwa kutoka nje ya Zanzibar na kutakiwa kuripoti ofisini kwa OCD kila siku saa tatu kamili asubuhi.**

Mkurugenzi huyo aliripoti ofisini kwa Mkuu wa Wilaya akiambatana na Mkandarasi wa mradi huo ambaye alizuiliwa kutoka nje ya Zanzibar na kutakiwa kuripoti ofisini kwa OCD kila siku saa tatu kamili asubuhi na kufanya hivyo kwa siku zote tatu.

Mkurugenzi huyo aliomba radhi kwa kampuni yake kuchelewa kukamilisha mradi huo kwa wakati na kuahidi mbele ya serikali ya wilaya kuukamilisha mradi huo ndani ya kipindi cha mwezi mmoja na nusu.

Pia, wamekubaliana kwasasa mradi huo utasimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kutakiwa kuwasilisha maendeleo ya mradi huo kila siku ya Jumatatu asubuhi mpaka hapo utakapokamilika.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B, Rajab, amemtaka Mkurugenzi huyo na Mhandisi wake kuhakikisha wanakamilisha na kutekeleza makubaliano yote yaliyofikiwa na kukamilisha mradi kwa wakati waliopangiwa.

Mradi huo wa tangi la kuhifadhia majisafi na salama katika kijiji cha Kitope, upo chini Mhandisi kutoka Kampuni ya Grative Tanzania Limited, Goodluck Jackson Kyaro na kusimamiwa na Taasisi ya Tanzania Youth Icon kwa ufadhili wa Taasisi moja ya Umoja wa Mataifa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed (kulia), akimpokea Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Idd, baada ya kuwasili kwenye viwanja vya ukumbi wa Sheikh Idris Abdul Wakil, mjini Unguja jana, kwaajili ya kupokea msaada wa vifaa vya kujikinga na mambukizi ya virusi vya Corona vilivyotolewa na Rostam Aziz vyenye thamani ya Sh. milioni 500 kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# ZAWA yataka taarifa kupasuka mabomba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeitaka jamii kutoa taarifa za kupasuka mabomba ya maji katika maeneo yao husussani katika kipindi hiki cha mvua inayoendelea kunyesha nchini.

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Ofisa Uhusiano wa ZAWA, Amina Abdala, alisema katika kipindi hiki kumekuwapo na uvujaji wa maji kwa baadhi ya mabomba ya zamani hali inayopelekea muda mwingine kuchanganyika na maji ya mvua yanayopita ardhini.

Alisema changamoto hiyo imewahi kujitokeza katika maeno ya Shaurimoyo na Mwembeladu na Mamlaka hiyo kuchukua hatua ikiwamo kuyarekebisha yaliyopasuka na kutiririsha maji ardhini ili kunusuru hali ya kuchanganyika na maji ya mvua.

Alisema Mamlaka hiyo imekuwa na utaratibu wa kupita katika maeneo mbalimbali kukagua mambo ya maji uhusussani ya muda mrefu ambayo yanapasuka na kuvujisha maji.

Vile vile, akizungumzia hali ya maji kuwa na vumbi katika baadhi ya maeneo katika kipindi hiki cha mvua, alisema tatizo hilo linatokana na chemchem ya maji iliyopo maeneo ya Mtopepo kujaa maji kwa kupitiliza hali inayosababisha hata maji yanayosambaa majumbani kuwa na vumbi.

"Kesi za maji kuwa kama na vumbi kwa wakati huu wa mvua hii inasababisha baadhi ya vyanzo vya maji kuwa na maji mengi kupita hali yake ya kawaida na ndio maana tunaendelea kutoa elimu ya kuchemsha maji ya kunywa na kuweka dawa ili kujikinga na maradhi ya mripuko licha ya Mamla ya maji kuendelea kuchukua hatua," alisema.

Aliwaomba wananchi kwenda kuchukua dawa za kuweka katika maji na wenye visima vyao binafsi wanatakiwa kuchukua dawa hizo ili kujikinga na maradhi ya mlipuko ikiwamo kuumwa matumbo hususani katika kipindi hiki.

# Tume ya Utangazaji yaonya wanaotangaza uzushi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TUME ya Utangazaji Zanzibar imetoa onyo kwa watu wenye tabia na desturi za kutangaza habari za uzushi na zisizofanyiwa utafiti wa kitaalamu kupitia mitandao ya kijamii jambo ambalo linapelekea kutia hofu kwa jamii.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Omar Said Ameir, alisema onyo hilo pia linawahusu wanaopelekewa taarifa za uongo na baadaye kuanza kuzisambaza kupitia kurasa zao za mitandao ya kijamii kinyume cha sheria za tume hiyo.

Alisema hivi karibuni, imezuka tabia ya baadhi ya watumiaji wa mitandao ya kijamii kurusha taarifa mbali mbali zisizo na ukweli ikiwamo kukashifu baadhi ya viongozi wa serikali hali inayosababisha jamii kuwa na hofu na wasiwasi kiasi cha kuonekana tume hiyo haifanyi kazi yake kama inavyotakiwa.

"Zipo kurasa za mitandao ya kijamii ambazo kazi yake kubwa kuwachafua viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hata baadhi ya wanasiasa, wanaandika taarifa za uongo ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kihabari kama inavyotakiwa hii sio sahihi, kutoa taarifa ya uongo ni kosa, zipo njia za kupata taarifa nadhani kama umesoma vizuri uandishi basi huwezi kufanya makosa kama haya," alisema.

Vile vile, alisema kuwa Tume hiyo imeanza kuwachukulia hatua za kisheria dhidi ya wote wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii ikiwamo kufanya vitendo hivyo viovu kwa kuandika taarifa za uongo dhidi ya viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikilenga kuwatia hofu wananchi ambao kwa asilimia kubwa wanatumia mitandao hiyo.

Hata hivyo, aliitaka jamii kujiepusha kwa kuandika mambo ambayo yataleta hofu nchini na badala yake wafuate taarifa zinazotolewa na serikali kupitia vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini.

**Onyo hilo pia linawahusu wanaopelekewa taarifa za uongo na baadaye kuanza kuzisambaza kupitia kurasa zao za mitandao ya kijamii kinyume cha sheria za tume hiyo.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN JUMA ODONGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI yenye namba za usajili **MC414 AMH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/323908/2020**

115709002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;88/2020**

**Ombi la ESROM P. MAKALA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALUM OMARY MAKALA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/03/2020.

Sahihi ya Hakimu

115709102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA**

**YAH: SHAURI LA MADAI NAMBA 80 / 2020**

**MDAI..................KISYERI WAMBURA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA…….…...DONATUS H. MASEKE**

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 22/04/2020 saa 2:00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani
Endapo hutafika mahakamani shauri litasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

*D.J.Butambala*
HAKIMU MKUU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA.

115708502

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DOREEN JOSEPH MINJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 417DPM.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/316721/2020**

115708301

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JUDITH ELIREHEMA MARICK** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 386 DLE.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/316716/2020**

215708402


***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la Nipashe***

***kila siku Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waliofariki kwa corona Ulaya wafikia 100,000

**LONDON,** Uingereza

VIFO vitokanavyo na ugonjwa wa virusi vya corona katika mataifa ya Ulaya vimefikia 100,000.

Bara la Ulaya ndilo limeathirika kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na mabara mengine duniani. Takriban watu 2,281,334 wamepata maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo hadi sasa duniani kote.

Mataifa ya Ulaya yamekabiliwa na vifo vya watu 100,510, idadi ambayo ni theluthi mbili ya watu wote 157,163 waliofariki duniani kutokana na ugonjwa huo kwa mujibu wa Shirika la habari la Ufaransa (AFP).

Hata hivyo, karibu robo ya vifo vilivyotokea ulimwenguni kote vimetokea nchini Marekani ambapo watu wapatao 38,000 wamekufa, kulingana na chuo kikuu cha John Hopkins.

**Iran imeruhusu biashara kadhaa za mjini Tehran kufunguliwa tena milango yake siku ya Jumamosi.**

Zaidi ya watu bilioni 4.5 wanaendelea kubaki majumbani kama sehemu ya juhudi zinazochukuliwa kwa hiari au za lazima ili kupunguza kuenea kwa maambukizi ya virusi vya corona.

Nchi za Japan, Mexico, Hispania, Ufaransa, na Uingereza ni kati ya nchi ambazo zimeweka hatua hizo au hata kurefusha muda wa watu kubakia majumbani.

Uswizi, Denmark na Finland zimetangaza kwamba maduka na shule zitafunguliwa tena kuanzia wiki ijayo.

**MAREKANI**

Huko Marekani, Rais Donald Trump, ametangaza kuwa hatua hizo zitaanza kulegezwa katika majimbo ya Texas na Vermont kuanzia Jumatatu.

Maandamano yalifanyika ambapo watu walikuwa wanapinga amri ya kutoka nje ambayo wanadai imeathiri uchumi wa nchi hiyo.

**UJERUMANI**

Ujerumani kwa upande wake, imetangaza kuvidhibiti virusi hivyo baada ya watu 3,400 kufa kutokana na ugonjwa huo na itaanza kulegeza baadhi ya hatua zilizowekwa kwa tahadhari kubwa.

Baadhi ya maduka yameruhusiwa kufungua milango yake kuanzia Jumatatu, na baadhi ya watoto wataweza kurudi shuleni katika kipindi cha wiki moja ijayo.

**ITALY**

Kwingineko, Italia pia imeanza kupunguza makatazo na wakazi wa mji wa Venice walionekana nje wakipunga hewa.

**IRAN**

Iran imeruhusu biashara kadhaa za mjini Tehran kufunguliwa tena milango yake siku ya Jumamosi.

Dalili za kudorora kwa uchumi wa dunia unaosababishwa na janga la corona zinaendelea kujitokeza. China imetangaza kupungua kwa pato la taifa la nchi hiyo kwa mara ya kwanza tangu kujitokeza hali kama hiyo mnamo miaka ya 90. **DW**



Baadhi ya wananchi wa Uingereza, wakiwa wamevalia Barakoa kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: ALLIANCE**

## Rais aondoa marufuku watu kutoka nje

**ACCRA,** Ghana

RAIS wa Ghana, Nana Akufo-Addo, ameondoa marufuku ya watu kutoka nje katika baadhi ya maeneo ya nchi hiyo, ambayo yalikuwa yamefungwa ili kudhibiti kusambaa kwa virusi vya corona.

Lakini, wananchi wa taifa hilo watatakiwa kuvaa barakoa , na makatazo kama kufungwa kwa shule na mikusanyiko ya watu bado yatakwapo.

Mipaka ya nchi hiyo pia itaendelea kufungwa kwa wiki mbili zaidi wakati mapambano dhidi ya virusi vya corona yakiendelea.

Rais Akufo-Addo alisema uamuzi huo umekuja baada ya uelewa mzuri wa kasi ya maambukizi na programu kubwa ya kupima watu na kutanua vituo vya kutenga watu pamoja na matibabu.

Mji wa Accra, Kumasi pamoja na Jiji la viwanda la Tema yaliwekwa katika marufuku ya watu kutoka nje kwa wiki tatu ili kuzuia maambukizi ya virusi vya corona. **BBC**

## Dereva aliyesafirisha jeneza feki akamatwa

**NAIROBI,** Kenya

JESHI la Polisi nchini Kenya, limemkamata dereva aliyekuwa na abiria watatu waliojidai kuwa waombolezaji wanaoelekea kwenye mazishi.

Watu hao waliokuwa wamesafiri zaidi ya kilomita 370 kutoka Nairobi wakiwa wamebeba jeneza tupu walikamatwa katika jimbo la Homa Bay magharibi mwa nchi hiyo.

Waziri wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa watu hao walifanikiwa kuwahadaa polisi na kupita vizuizi kadhaa wakiwa na jeneza hilo.

Kagwe aliongeza kuwa dereva huyo ametengwa na abiria wake watatu kuwekwa karantini.

Alisema serikali inachunguza madai kwamba baadhi ya watu wanatoa hongo kwa polisi wanaosimamia vizuizi vya barabarani.

Kadhalika, uchunguzi huo utahusu mali ori yanayoenda safari za mwendo mrefu kutokana na madai ya kuwasafirisha watu kinyemela kutoka jijini Nairobi.

Wiki mbili zilizopita serikali ya Kenya ilitangaza hatua kali za kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona na kwamba iliweka marufuku ya usafiri wa kuingia na kutoka maeneo mengine matatu ambayo yanasadikiwa kuwa na viwango vya juu vya maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Hadi sasa Kenya ina wagonjwa 262 wa corona baada ya watu 16 wapya kuthibitishwa kuwa na virusi siku ya jumamosi.

Wakati huohuo, shughuli za biashara katika mtaa wa Eastleigh jijini Nairobi, zimesitishwa katika juhudi za kukabiliana na kusambaa kwa virusi vya corona.

Chama cha wafanyabiashara wa Eastleigh kimesema hatua ya kufunga maduka ilichukuliwa baada ya kubainika kuwa wafanyabiashara wameshindwa kuzingatia muongozo uliotolewa na wizara ya afya, kama vile watu kutokaribiana na kunawa mikono ama kuvaa barakoa. **BBC**

## Waandamana kupinga kukaa ndani

**NEWYORK,** Marekani

WAANDAMANAJI nchini Marekani, wameingia mitaani katika majimbo kadhaa wakishinikiza magavana kufungua uchumi wa majimbo yao pamoja na kuondoa amri ya kutokutoka nje.

Marufuku ya kutokutoka nje imewekwa katika majimbo yote ya Marekani ili kudhibiti kusambaa kwa virusi vya corona, hali iliyotikisa uchumi wa taifa hilo kubwa zaidi kiuchumi duniani.

Maandamano hayo yameripotiwa juzi katika majimbo ya Arizona, Colorado, Montana na Washington, huku mwendelezo wa maandamano hayo ukitarajiwa leo

Hasira juu ya marufuku hizo imeongezeka nchini humo huku waandamanaji wakitaka masharti yalegezwe licha ya hatari ambayo yamewekwa ya ugonjwa huo.

Rais wa Marekani, Donald Trump alionesha dalili za kukubaliana na maandamano hayo.

Kwa sasa, Marekani ndiyo kitovu cha ugonjwa wa virusi vya corona, kukiwa na wagonjwa zaidi ya 735,000 na vifo zaidi ya 40,000.

Hata hivyo, kuna dalili kuwa maambukizi yanafikia kileleni nchini humo na kasi ya maambukizi kuanza kushuka katika baadhi ya majimbo.

Magavana katika majimbo mbalimbali wameanza majadiliano ya kufungua uchumi baada ya kushuhudiwa kupungua kwa maambukizi, lakini maeneo mengine bado yangali kwenye marufuku kali. **BBC**




# ROONEY AMTABIRIA KANE MAKUBWA ENGLAND

**LONDON,** England

WAYNE Rooney anaamini Harry Kane atavunja rekodi ya kufunga mabao katika Timu ya Taifa ya England.

Rooney alisema ubora wa mshambuliaji huyo wa Tottenham Hotspur unamweka katika nafasi nzuri ya kuvunja rekodi ya kufunga mabao zaidi England.

Nahodha huyo wa zamani wa Manchester United na England, anashikilia rekodi ya kufunga mabao 53 katika mechi 120 alizoichezea Timu ya Taifa.

Kane ambaye ndiye nahodha wa England kwa sasa, amefunga mabao 32 katika mechi 45 alizocheza za timu hiyo. Licha ya kucheza Marekani kabla ya kurejea England kujiunga na Derby ya daraja la kwanza, nguli huyo bado anashikilia rekodi ya kufunga mabao.

"Lazima niwe mkweli na inaweza kukushangaza, lakini mimi si mfungaji bora asilia. Kushikilia rekodi ya ufungaji Manchester United na England ni jambo la kujivunia,"alisema Rooney akinukuliwa na Sky Sport.

# Kante kubadilishwa na Coutinho

**LONDON,** England

KLABU ya Barcelona imeripotiwa kuwa kwenye mazungumzo na Chelsea ili kubadilishana wachezaji, Philippe Coutinho na N'Golo Kante.

Kwa mujibu wa gazeti la AS la nchini Hispania, Barcelona imekuwa ikimtazama Kante kwa muda mrefu hivyo kwa msimu huu inataka kuhakikisha inaipata saini yake ili kwenda kufanya maboresho katika kikosi chake.

Lakini upinzani mkubwa unaonekana kwa Real Madrid ambayo nayo inaonekana kumtamani mchezaji huyo.

Kabla ya taarifa za Barcelona kutaka kubadilishana na Chelsea, hapo mwanzo Chelsea ilikuwa inahitaji kumchukua kwa dili la mkopo Coutinho, ikiwa ni pamoja na kulipa mshahara wake wa pauni 250,000 kwa wiki.

Lakini mambo yanaonekana kubadilika na huenda mchezaji huyo akajiunga na matajiri hao wa London kwa dili la moja kwa moja.







# United yaendelea kumkomalia Sancho

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imejipa matumaini ya kushinda kwenye mbio za kuwania saini ya Jadon Sancho.

Sancho ameteka vyombo vya habari Ulaya baada ya kuzivutia idadi kubwa ya klabu zinazotaka kumsajili wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto.

United ina matumaini kumpata Sancho baada ya kuteta na klabu yake ya Borussia Dortmund na mchezaji husika.

Klabu hiyo italazimika kufanya kazi ya ziada kupata saini yake kwa kuwa Dortmund imepanga kumwongeza dau la mshahara ili kumbakiza.

Thamani ya Sancho inadaiwa kufikia pauni milioni 100 katika usajili wa majira ya joto unaokuja.

Sancho amekuwa katika kiwango bora tangu alipotua katika Ligi Kuu Ujerumani akifunga mabao 17 na kutengeneza mengine 19 msimu huu.

## HABARI MICHEZO

# Juve yajitoa kumwania Hary Kane

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeripotiwa kuingia kwenye mbio za kuwania saini ya mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Hary Kane, ambaye anahusishwa kutaka kuondoka klabuni hapo katika dirisha linalokuja la majira ya joto.

Taarifa kutoka Italia zinadai Juve wameingia kwenye mbio hizo kwa kile kinachoelezwa kwamba mshambuliaji wao Gonzalo Higuain anataka kutimka kwenye klabu hiyo.

Kwa sasa Higuain yupo kwao Argentina kumwangalia mama yake anayesumbuliwa na maradhi ya saratani, lakini taarifa zinadai kwamba straika huyo huenda asirudi kabisa kujiunga na miamba hiyo ya Italia.

Mchezaji huyo inabidi arudi wiki ijayo ili kuingia karantini kwa siku 14 kabla ya kuanza mazoezi, lakini taarifa zinadai kwamba amekaidi na kitendo hicho kinaweza kusababisha kuvunjwa mkataba wake ambao unamalizika Juni 2021.

Na sasa Juve imeamua kuingia kwenye mbio hizo za kupigana vikumbo na klabu kadhaa barani Ulaya katika kuwania saini ya Kane.

Licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kwa msimu huu hajacheza mechi nyingi zaidi kutokana na majeruhi yaliyokuwa yanamwandama, hadi sasa amefunga mabao 17 katika michezo 25.





# GIROUD AFIKIA MWAFAKA NA INTER

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI Olivier Giroud, amefikia mwafaka kuhusiana na maslahi binafsi na Inter Milan inayotaka kumsajili katika majira ya joto.

Taarifa za awali zimedai mshambuliaji huyo wa Chelsea atatua San Siro kwa mkataba wa miaka miwili.

Conte aliwahi kumtupia ndoano Mfaransa huyo katika usajili wa dirisha dogo Januari, mwaka huu.

Mshambuliaji huyo anasaka timu baada ya kupokwa namba na kinda Tammy Abraham.

Tammy anaonekana kuwa chaguo la kwanza kwa kocha Frank Lampard na Inter inaweza kupata saini ya Giroud akiwa mchezaji huru majira ya joto.

# *Chelsea wakubali kukatwa mishahara*

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Chelsea, wamekubali kukatwa asimilia 10 ya mishahara yao katika kipindi hiki cha janga la virusi vya Corona.

Nyota hao wamefanya majadiliano na kukubaliana kupitia kundi lao la mtandao wa kijamii la whatsApp, wakiongozwa na nahodha, Cesar Azpilicueta.

Gazeti la Daily Mail mwishoni mwa wiki liliripoti wachezaji wa Chelsea walikuwa wanajadiliana namna ya kukatwa mishahara na tayari wamefikia muafaka, ingawa bado haijathibitishwa na uongozi wa juu wa klabu kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji, Marina Granovskaia.

Wakati huo huo, Umoja wa Wachezaji wa Ligi Kuu England, wameripotiwa kukusanya pauni milioni 4 kwa ajili ya kuchangia huduma za afya katika kipindi hiki cha kupambana na virusi vya corona.

Fedha hizo zitawasaidia wahudumu wa afya walio mstari wa mbele kupambana na virusi vya Corona na maeneo mengine yenye uhitaji mkubwa.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AANDALIWA MSHAHARA 'KUFURU'

● ● ● Lengo ni kukacha mpango wa kurejea Barcelona na kumshawishi abakie jijini Paris...

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain inajiandaa 'kumpatia Neymar mkataba mpya wenye dau kufuru la pauni milioni 33 kwa mwaka' ili kumshawishi nyota huyo akatae mchakato wa kurejea Barcelona.

**Kwa muda mrefu mchezaji huyo nyota wa Timu ya Taifa ya Brazil amekuwa akihusishwa na mpango wa kurejea Nou Camp, ambapo alichezea Barcelona kati ya mwaka 2013 na 2017 kabla ya kutua jijini Paris kwa dau lililoweka rekodi ya dunia ya pauni milioni 198.**

Lakini kwa mujibu wa gazeti la michezo la Hispania liitwalo Diario Sport, Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo, anatarajia kufanya kila linalowezekana ili kumbakisha mshambuliaji huyo klabuni hapo hadi mwaka 2025 kwa kumpa mkataba mpya ambao atalipwa mshahara wa pauni 640,000 kwa wiki.

Mkataba huo mpya utamfanya Neymar akaribie mishahara ya wachezaji soka wawili maarufu ambao wanalipwa zaidi yake ambao ni, Lionel Messi wa Barcelona na Cristiano Ronaldo anayeitumikia Juventus.

Neymar amefunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho 10 katika mashindano mbalimbali, ambayo PSG wamecheza msimu huu kabla ya michezo kusimama kufuatia majanga ya virusi vya ugonjwa wa corona (Covid-19).

Mkataba wake wa sasa ambao analipwa mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki unatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2022 na endapo mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atakubali kusaini mkataba mpya 'atazima' tetesi za kurejea Barcelona.

Tayari Neymar ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa katika kikosi hicho cha Parc des Princes kwa kuwaacha wenzake mbali, huku mshambuliaji mwenzake mwenye umri wa miaka 21, Kylian Mbappe akifuatia kwa kulipwa pauni 375,000 kwa wiki, limeandika gazeti la L'Equipe.

Kwa kipindi cha mwezi mmoja sasa taarifa mbalimbali huko Hispania zinaandika Barcelona inajiandaa kumrejesha Neymar na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, katika majira ya joto.

Lakini maambukizi ya virusi vya corona yameitikisha klabu hiyo ya Katalunya, huku tayari ikiwalipa wachezaji wake asilimia 70 ya mshahara wanaopata.

PSG iko kileleni katika msimamo wa Ligue 1 ikiwa imeizidi pointi 12 Marseille na inajiimarisha ili kutetea taji hilo la ubingwa wa Ufaransa wakati bado msimu umesimama.

## ZISIKUPITE

### JUVE YAACHANA NA KANE

JUVENTUS imesitisha uamuzi wake wa kufuatilia saini ya straika wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### MADRID YAJITOA

REAL Madrid imejiondoa kwenye mbio za kuwania saini ya straika wa Timu ya Taifa ya England na Spurs, Harry Kane (26), kwa sababu ya tatizo la fedha lililotokana na kuwapo kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona ( COVID 19). ***(Mail)***

### MADRID KUUZA SITA

MABOSI wa Real Madrid, wanajiandaa kuuza wachezaji wao sita wa kikosi cha kwanza akiwamo winga wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (30), na kiungo wa Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez, ambaye ana umri wa miaka 28. ***(AS)***

### ARSENAL KUMTOA LACAZETTE

ARSENAL inatarajia kumtoa mshambuliaji Mfaransa Alexandre Lacazette (28), kama sehemu ya kufanikisha kiungo wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Party (26) anajiunga na The Gunners. ***(Sun)***

### MORENO ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kumsajili winga wa Valencia na Timu ya Taifa ya Hispania, Rodrigo Moreno ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

### ARSENAL, UNITED VITANI

ARSENAL na Manchester United zinajipanga kufanya mchakato wa kuwania saini ya mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Sport - in Spanish)***

### HAVERTZ AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United imemwongeza kiungo wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Kai Havertz (20), katika orodha ya wachezaji inaowahitaji katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Standard)***

### WALDSCHMIDT SOKONI

CHELSEA inajiandaa kutoa kiasi cha pauni milioni 20 ili kumsajili straika wa Freiburg na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Luca Waldschmidt (23). ***(Sun)***

### GIROUD MAMBO SAFI

STRAIKA wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud (33), amefikia makubaliano na klabu hiyo kuhusiana na maslahi yake ili abakie Inter Milan. ***(Tuttosport via Mail)***

### NASRI MATATANI

KIUNGO wa zamani wa Manchester City na Arsenal, Samir Nasri (32), anajiandaa kutimuliwa na Anderlecht baada ya kushindwa kuwasiliana na mabosi wake katika kipindi hiki cha maambukizi ya ugonjwa wa corona. ***(Derniere Huere via Mail)***

### KEAN ATAKIWA INTER

INTER Milan iko tayari kutoa dau la pauni milioni 25 kwa Everton ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Italia, Moise Kean, ambaye ana umri wa miaka 20. ***(Express)***

## Njaa yawakimbiza wachezaji Bweleo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HALI ya ukata umewafanya wachezaji wa Bweleo Warrious 'kukacha' mazoezi ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Said Mohammed, alisema kikosi hicho kina wachezaji 27 lakini nyota wanaohudhuria mazoezi ni nane tu.

Mohammed alisema hali ya 'ukata' imesababisha timu yao kufanya vibaya katika msimu huu na sasa wanachofanya ni kuendelea kupambana ili wasishuke daraja.

"Tuna changamoto ya kukosa fedha, tumeshindwa kusajili wachezaji wazuri na waliopo pia tunashindwa kuwalipa mishahara kwa wakati," alisema Mohammed.

Aliongeza timu hiyo pia haina vifaa vya mazoezi na hali inayomweka kwenye mazingira magumu kocha wao.

"Klabu haina fedha, kuna muda mwingine tunashindwa kutimiza hata mahitaji ya vifaa anavyohitaji kocha wetu, hii ni hatari, ili timu iweze kufanya vizuri unahitaji kuihudumia kwa kumpatia mwalimu vifaa na kuwalipa wachezaji mishahara yao ili kuongeza morali,"alisema kiongozi huyo.

## Fulgence atamani kuzeekea Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, amesema anatamani kuona anafundisha kwa muda mrefu kwenye timu za Ligi Kuu Bara, lakini kushindwa kudumu kwenye klabu hizo kunatokana na sababu ambazo ziko nje ya uwezo wake.

Fulgence ameiongoza vyema Gwambina FC ya jijini Mwanza ambayo inashiriki Ligi Daraja la Kwanza kwa kukaribia kupanda daraja.

Kocha huyo aliliambia gazeti hili aliondoka Stand United ya Shinyanga iliyokuwa Ligi Kuu kutokana na kulazimika kurejea darasani kwa kushiriki kozi ya juu iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), na kuwalazimu viongozi wa timu hiyo kusaka kocha mwingine.

"Kipindi namaliza masomo, viongozi wa Stand tayari walikuwa wameshaingia mkataba na kocha mwingine ambaye aliisaidia katika mchakato wa usajili, nikalazimika kuelekea Singida United, napo sikukaa kwa muda mrefu na kujiunga na Kimondo iliyokuja na ofa nzuri kwangu," alisema Fulgence.

Aliongeza hata hapo Kimondo pia hakukaa kwa muda mrefu na alijiunga na Namungo ya Lindi, ambayo nayo ilipopanda Ligi Kuu, iliajiri kocha mwingine baada ya yeye kubanwa na majukumu ya Timu ya Taifa.

# MBEYA CITY YAZIFUATA SIMBA, YANGA KAMPUNI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya City, umesema tayari wamefanikiwa kupata usajili mpya wa timu hiyo ambao utawaruhusu kuanza mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, alisema maombi ya kubadilisha usajili yalianza kufanyika tangu mwaka 2018 na sasa wanajiandaa kuanza mchakato wa kuiendesha klabu hiyo kwa mfumo wa kampuni.


Kimbe alisema watafuata taratibu zote za mabadiliko ya uendeshaji kama serikali inavyoelekeza na wanaamini baada ya kukamilisha kwa mchakato huo, timu yao inapata wawekezaji ambao watasaidia shughuli za kiutawala na kurejea kwenye ushindani.

**"Malengo yetu ni kufanya Mbeya City kuwa kampuni, tayari usajili umekamilika, ila lini tutaanza kazi ndio mtihani, kwa sababu suala hili lina taratibu zake ikiwamo kufuata taratibu zilizowekwa na nchi," alisema Kimbe.**

Katibu huyo alisema uongozi umeamua kufanya mabadiliko hayo ili kurahisisha kukaribisha wawekezaji pamoja na kampuni na taasisi binafsi ili kusaidia kudhamini na hatimaye watafikia malengo ya kukuza na kuendeleza vipaji vya soka nchini.

"Kuna mahali ilikuwa tunakwama kupata ushirikiano kwa sababu timu hii ilionekana ni ya serikali ya mkoa, sasa tutakuwa huru na tutawakaribisha wawekezaji ili kuingia ubia," Kimbe alisema.

Tayari mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba, wameshaanza mchakato wa kubadilisha mfumo wa uendeshaji na watani zao, Yanga wameanza maandalizi ya kuelekea katika mfumo huo ambao utaruhusu wawekezaji na wanachama kununua hisa.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kulia), akisalimiana na wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), waliokuwa wanajiandaa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali zilizopita za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019). **PICHA: MAKTABA**

# *Kocha wa Simba, Prisons afariki*

**Na Saada Akida**

ALIYEWAHI kuwa kocha wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam na Tanzania Prisons ya Mbeya, David Mwamwaja (pichani), amefariki dunia jana asubuhi katika hospitali ya Tumbi iliyoko Kibaha, Pwani.



Akizungumza na gazeti hili jana, mke wa marehemu Mwamaja, Mary Mwamwaja, alisema mume wake alifariki jana asubuhi katika hospitali hiyo baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Mary aliliambia gazeti hili wiki iliyopita marehemu aliugua malaria na aliendelea vizuri, lakini juzi usiku hali ilibadilika na kusababisha kurudishwa hospitali ili kupata matibabu.

"Alianza kujisikia vibaya, tukampeleka katika hospitali ya Meddwell (iko Kibaha pia), lakini madaktari walitoa maelekezo ya kumpeleka Tumbi baada ya kuona hali sio nzuri," alisema mke wa marehemu.

Aliongeza bado familia haijapata taratibu za mazishi za nyota huyo wa zamani wa timu ya Kurugenzi na Kombani ya Mkoa wa Arusha (Meru Warriors).

Marehemu Mwamwaja aliwahi pia kufundisha klabu za Bandari ya mkoani Mtwara, AFC (Arusha) na JKT Tanzania ya jijini.

Michezo

Jumanne Aprili 21, 2020

Nipashe



Neymar aandaliwa mshahara 'kufuru'

UKURASA 22

FURAHA YA USHINDI..




Wachezaji wa Manchester United, Paul Pogba (kushoto) na Jesse Lingard, wakishangilia bao katika moja ya mechi za Ligi Kuu England mapema mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## Pondamali awaita Yanga Kandambili

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA nyota wa zamani wa Yanga, Pan Africans na Timu ya Taifa ( Taifa Stars), Mohammed Adolf, amesema golikipa mkongwe wa timu hiyo, Juma Pondamali ndiye mwasisi wa jina la Kandambili.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Adolf ambaye kwa sasa ni Kocha Mkuu wa Prisons, alisema jina la Kandambili lilitokana na mpasuko uliotokea ndani ya Yanga mwaka 1974, ambao ulichangiwa na ya viongozi kupendekeza waliokuwa baadhi ya wachezaji 'wakubwa' wafukuzwe.

"Basi baada ya kuwa na mvurugano, Juma Pondamali "Mensah" alisimama juu pale Jangwani na kuwaaita waliokuwapo ni Kandambili," alisema Adolf akielezea jina hilo wanalotaniwa Yanga lilipotokea. Adolf alisema bado anaikumbuka mechi zote walizocheza na Zambia, na kueleza wapinzani wao walionyesha kiwango cha juu katika mechi zote mbili.

"Dakika 45 za kwanza tulishambuliwa haswaa, siku ile Pondamali alidaka sana, walikuwa wanaweza, wanaujua mpira, walikuwa na ubora wa hali ya juu, ila Tino (Peter), alikuwa anajua mpira, anajua sana kumalizia, mguu wake ulikuwa na uwezo wa kufunga upande wowote, ulikuwa na hisia za kufunga, alikuwa mjanja mjanja," Adolf alisema.

Nyota huyo ndiye alifunga bao la ushindi wa 1-0 katika mechi ya kwanza hapa nyumbani kati ya Taifa Stars dhidi ya Zambia na Peter Tino alisawazisha bao wakiwa ugenini baada ya Alex Chola kuifungia Chipolopolo kwenye mchezo wa marudiano.

# Simba, Yanga zatambiana

**Na Somoe Ng'itu**

## ●●● Kila upande waonyesha jeuri ya fedha katika mbio za kunasa 'majembe' kuelekea msimu mpya...

KATIKA kuhakikisha kila timu inajiimarisha kuelekea msimu mpya, viongozi wa klabu za Simba na Yanga wametamba kusajili kila mchezaji 'mzuri' atakayetakiwa na benchi la ufundi kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi Mipango wa Kampuni ya GSM, inayowadhamini Yanga, Hersi Said alisema klabu hiyo imejipanga kuwasajili wachezaji wote watakaopendekezwa na Kocha Mkuu wa timu yao Mbelgiji Luc Eymael.**

Said alisema Yanga itakamilisha kwa asilimia 100 mipango na mapendekezo yaliyoainishwa katika ripoti ya ufundi ya Eymael na malengo ni kuona msimu ujao wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na vile vile kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa.

"Tumejipanga kukamilisha kwa ufanisi mipango ya mwalimu wetu, tutafanikisha mapendekezo yote aliyoyatoa, tutamsajili kila mchezaji tunayemhitaji, tutasajili kila mchezaji aliye katika mipango ya mwalimu, tunaahidi hilo kwa Wanayanga," alisema Said.

Aliongeza Yanga pia itahakikisha inawabakisha wachezaji wa zamani ambao bado kocha anawahitaji na vile vile kujaza nafasi za watakaoachwa kwa umakini.

Hata hivyo kiongozi huyo alikataa kutaja nafasi ambayo wataziboresha kwa ajili ya msimu mpya baada ya kuona msimu huu nafasi yao ya kutwaa ubingwa imekuwa finyu.

"Siwezi kusema tutasajili nafasi zipi, hata Chama (Clatous), siwezi kumzungumzia kwa sababu ni mchezaji ambaye bado ana mkataba na Simba, tutakamilisha maingizo yote tuliyoyalenga," Said alisisitiza.

Naye Ofisa Mtendaji wa Simba, Senzo Mbatha aliliambia gazeti hili klabu yake inaendelea na skauti ya wachezaji wapya na ina uwezo wa kusajili nyota yoyote wa hapa nchini endapo watamhitaji.

"Tunaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu, ila mpaka sasa hakuna mchezaji ambaye tumeshazungumza naye, ila kwa wachezaji wa hapa Tanzania, yoyote tunayemhitaji hatutashindwa kumsajili," alisema ofisa huyo.

Katika kuhakikisha kila klabu inalinda nyota wake, tayari Yanga imeshawaongezea mikataba wachezaji wake, Papy Tshishimbi na Bernard Morisson, ambao walitajwa kuwindwa na Simba huku vinara hao wa Ligi Kuu wakisitisha mpango wa watani zao kumsajili, Hassan Dilunga.

Simba pia imefanikisha kumbakisha klabuni hapo mshambuliaji wake tegemeo Mnyarwanda Meddie Kagere ambaye alikuwa anawindwa na Levante inayoshiriki La-Liga ya Hispania kwa dau la Sh. milioni 150.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama katika raundi ya 28, Simba yenye pointi 71 ilikuwa inaongoza katika msimamo huku pia ikiwa imetinga katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA, ambayo bingwa wake hukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >